
SUPA JACKPOT
TZS. 1,152,911,993
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



**Makofi** ya shavuni, meno kung'olewa holela chanzo cha mtoto kuwa kiziwi

UKURASA 3


ama
ALHAMISI SEPTEMBA 14, 2023
AFYA NA MAZINGIRA

Ukurasa 14

Mila na desturi zinavyowaweka hatarini wajawazito wakitelekeza huduma kliniki

Huduma mpya Afya kwa Wote, ilivyokitanzi kwa haki ya mtoto

Ukurasa 12

KUTAPAKAA UKATILI KONA ZOTE…

Madhila ya elimu duni, tamaa na umasikini inavyowazamisha vijana

Na Yasmine Protace

MFUMO wa maisha sasa unatajwa kuwa kikwazo kwa watoto wa kike na kiume kufanyiwa vitendo vya ukatili wa kijinsia, ambao watoto wa kike wanabakwa, pia wako wanaonajisiwa.

Mwenyekiti wa Kituo Cha Taarifa na Maarifa, Mabibo Dar es Salaam, Rehema Mwinyi, anataja ukatili wa kijinsia unatokana na sababu mbalimbali, ikiwamo mfumo wa maisha ya kila siku.

Anasema, kutokana na kituo chao kuwasaidia wanaofanyiwa ukatili wapate haki, kuna uchunguzi unaofanyika kwa baadhi ya wanaofanyiwa ukatili na kubaini mfumo wa maisha nao unachangia ukatili kufanyika ikiwamo, ndoa.

"Mfumo wa maisha,unakuta watoto wengi,wanakosa malezi,wanakosa chakula na hivyo,wanaamua kutafuta chakula kwa njia ambazo sio halali na hivyo kubakwa au kulawitiwa, ili waweze kupatiwa pesa," anasema.

Katika hilo, wanandoa wanapoachana husababisha watoto kujilea, nayo inachangia watoto kufanyiwa ukatili wa kijinsia.

Pia, uchunguzi umegundua sababu nyingine ni mimba za utotoni, mtoto anayezaliwa analelewa na mtu baki, wakiwamo wazee vijijini, hatua ambayo mtoto huyo anakuwa wa kujiamulia mambo yake, hata anafikia hatua kutojua mipaka kati ya yanayofaa na yasiyofaa kimaisha.

Anashauri elimu iendelee kutolewa, ili kuwanusuru watoto wasifanyiwe matukio ya ukatili, huku kukitajwa ukatili mwingine unaofanywa hasa kwa watoto wa kiume, kutokana na kukosa pesa za kuingia katika mabanda ya sinema, ikiwamo Sh. 200, ambayo ni mvuto mkubwa kwao.

Rehema anasema, sasa nguvu kubwa zinaelekezwa shuleni kwa kuwapatia elimu ya ya jinsia watoto na namna ya kujilinda, ili wasifanyiwe mabaya hayo.

Mtazamo wake ni kwamba, mfumo wa maisha unapobadilika, matukio ya ukatili nayo yanaweze ama kuisha au kupungua.

Anasema, katika ofisi zao huwa wanawapokea watu mbalimbali wenye malalamiko ya ukatili na kuchunguza ukweli, pia sababu za kufanyiwa ukatili huo.

Kaimu Mkurugenzi wa Shirika la Usawa wa Kijinsia Tanzania (SUKITA), Msafiri Mwajuma Mariam, ambaye pia ni Mkuu wa Dawati la Mafunzo na Uelimishaji SUKITA, anasema wanawapatia watoto elimu, jinsi ya kupambana na matukio ya kikatili.

Anaeleza shirika lao lililoanzishwa mwaka 2014, limeshabaini anachokifafanua kuwa ni; "Serikali iliweka nguvu kubwa kwa ajili ya kuwalinda watoto wa kike katika ukatili na wakawasahau watoto wa kiume."

Pia, Mariam anafafanua kutokana na nguvu kubwa kutumika kuwalinda mabinti, sasa adha hiyo inawaangukia watoto wa kiume zaidi, ambao wana kawaida ya kukaa kimya.

"Watoto wa kiume wanaofanyiwa ulawiti hawasemi, kwa kuwa wanaowalawiti wanawaambia wakisema watauawa," anasema.

" Watoto wa kiume wakikosa shilingi 200 kwa ajili ya kucheza 'gemu' au kuingia katika mabanda ya video, hulazimika kufanya mapenzi ili waweze kupata pesa hiyo," anasema.

Kutokana na madhila hayo ya ukatili, anasema taasisi yao imekuwa ikitoa elimu ya watoto jinsi ya kulinda na masuala ya ukatili wa kijinsia.

" Wanatoa elimu ili iwasaidie wanafunzi wawe mabalozi shuleni na sasa wana mpango wa kwenda sokoni, misikitini na makanisani kwa ajili ya kutoa elimu ya masuala ya ukatili," anasema.

Anaongeza kuwa changamoto anayoiona, ni baadhi ya watu kufanyiwa ukatili kijinsia na kushindwa kutoa taarifa au wengine kumalizia majumbani, ili kesi zisiendelee.

Mariam anasema, matukio ya ukatili wa kijinsia yanatokea baada ya wazazi kutengana na kusababisha watoto kujilea wenyewe.

" Chanzo cha wanawake kutelekeza watoto na kusababisha kukaa na mama wa kambo, nayo inachangia kufanyika ukatili kwa jamii," anasema, akitaja kuwapo kesi za wanawake kudai talaka ili wagawane mali

Anasema ni kitu kinachochangia kutokea tatizo la ukatili, pale watoto wanapoachwa bila ya malezi sahihi.

Katika mchango wao SUKITA, Mariam anasema wameweza kutoa elimu ya afya ya akili, kwa kuwa pia inabainika kuwa sehemu ya matukio hayo ya mauaji na wabakaji.

MZIZI WA TATIZO

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Macho kwa Jamii, pia Mwenyekiti wa Kituo cha Taarifa na Maarifa Manzese, Dar es Salaam, Theresia Lihanjala, anasema kukosekana kwa utii kwa Mungu na umasikini, kuna nafasi kubwa ya kutokea ukatili wa kijinsia.

Anasimulia kuwapo vijana wanaopata watoto bila ya kuwa na matarajio, hali inayowafanya kukosa mahitaji muhimu na kuamua kujiingiza katika uhusiano wa kimapenzi.

"Unakuta mtoto kazaa mtoto, kumtunza hawezi anamuachia mtoto wake mtu amlelee na mtoto anapokosa huduma za kimsingi anajiingiza katika uhusiano na hata kufanyiwa ukatili," anasema.

Anaongeza kuwa watoto wengi kutokuwa na malezi, hali inayowachangia kujiingiza bila ya kujua katika makundi yasiyofaa, hata kusababisha wakafanyiwa ukatili mbalimbali.

Hapo Theresia anatumia mfano ulioko Manzese Dar es Salaam anakofanyia kazi, 'mabinti mama' ni wengi; mtoto anakuwa na mtoto.

Katika hilo, anahitimisha kwa ushauri: "Elimu itolewe kwa mabinti mama... elimu hiyo ikitolewa,

Watoto wakiwa katika mijumuiko yao. Ustawi wao kimaisha, kwa kiasi kikubwa unategemea mifumo bora ya wazazi na walezi wanaowasimamia. PICHA: MAKTABA.

Inaendelea Uk. 13

UKURASA 11

# Nipashe

Alhamisi Septemba 14, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581433
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital
epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US

MIKOPO ASILIMIA 10

RIPOTI YA UCHUNGUZI

# Wakopaji waanika ulaji vigogo h'shauri

- **Wadaiwa** wana mtandao wa rushwa, asiye na ndugu, kupata mtihani... *Endelea ukurasa 4*

## YALIYOMO

UKURASA WA 2

**AJIRA 2,500 ZAJA MAKAA YA MAWE MCHUCHUMA**

MRADI wa uchimbaji wa makaa ya mawe Mchuchuma unatarajiwa kutoa ajira rasmi 500, ajira za...

UKURASA WA 3

**WAZIRI CHANA ASHAURI MBINU ZA KUKWEPA MIGOGORO KIMKATABA**

WAZIRI wa Sheria na Katiba, Pindi Chana, amezitaka serikali za mitaa na halmashauri kupata ushauri wa...

UKURASA WA 5

**WATOTO 500 WASUBIRI UPASUAJI MOYO JKCI**

WATOTO 500 wenye matatizo ya moyo wanasuburi kufanyiwa upasuaji wa moyo katika Taasisi ya...


Sh. bilioni 88 zilizokopeshwa na halmashauri kwa makundi maalum mwaka 2021/22

Ushonaji

Utengenezaji sabuni

## Wanasiasa waafikiana mambo 15 ya kufuata

UKURASA 2



## Biteko atua TANESCO na angalizo kali

UKURASA 2

MICHEZO YANGA YAIFUATA AL - MERRIKH KIBABE UK.24
KATUNI UK.6

# Biteko atinga TANESCO na angalizo kali

**Na Restuta James**

"WATANZANIA wanataka umeme, wote tuimbe wimbo mmoja, Watanzania tunataka umeme, hoja yao wanataka umeme. Sisi ni lazima tujali mchakato wa kuwapatia umeme na Watanzania wanajua TANESCO ndiye mleta umeme."

Huyo ni Naibu Waziri Mkuu ambaye pia ni Waziri wa Nishati, Dk. Dotto Biteko, alipozuru katika ofisi za Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Ubungo, mkoani Dar es Salaam jana kwa lengo la kujitambulisha kwa wafanyakazi wa shirika hilo.

Dk. Biteko katika hotuba yake kwa wafanyakazi hao, alitamka maneno 'Watanzania wanataka umeme' mara 32, akiwataka wafanyakazi na menejimenti ya shirika kuwa wabunifu na kufikiri namna ya kuwafikishia nishati hiyo Watanzania wengi ili iwasaidie kwenye shughuli za kiuchumi.

Alisema ameona ari na shauku ya wafanyakazi katika kutimiza malengo ya serikali, akitumia dakika 32:58 kuwasilisha hotuba yake iliyokuwa na utani kiasi na angalizo kali kwa watendaji ili kuondoa giza nchini.

Alisema ili kufanikisha hilo, Wizara ya Nishati itashirikiana na menejimenti ya TANESCO kuunganisha rasilimali zilizopo na maarifa kuwezesha upatikanaji umeme.

Alisema wakati mwingine shirika hilo linaweza kukumbana na changamoto zilizo nje ya uwezo wake katika kufikisha umeme kwa wananchi. "Hiyo sio hoja ya Watanzania, hoja yao wanataka umeme. Unaweza kusema Wizara ya Fedha fanya hivi, Watanzania hawamjui Wizara ya Fedha, wanajua TANESCO atupe umeme. Unaweza kusema hakuna barabara ya kupeleka nguzo, hawamjui TANROADS, wanamjua TANESCO ndiye mleta umeme, sijui tunaelewana jamani?" alihoji

Alisema ili kuondoa changamoto hizo, Wizara ya Nishati itaziunganisha taasisi zote zinazoingiliana na TANESCO, ili kupunguza lawama kwa shirika hilo na kurahisisha kazi ya kufikisha nishati hiyo kwa wananchi.

"Kazi hii hatutaweza kuifanya kama tutachukua muda mwingi kushughulika na watu badala ya hoja. Ukifika ofisini asubuhi unaposalimiana na mwenzako mwangalie usoni mwambie 'Watanzania wanataka umeme'," aliagiza.

Alisema anatamani kuacha alama katika wizara hiyo, lakini akiwa na angalizo "kama ninyi hamjanipa ushirikiano, Watanzania hawatapata wapate umeme."

Waziri Biteko alimwelekeza Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Felichism Mramba na Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Maharage Chande, kuwaunganisha wafanyakazi na kuondoa dhana ya makundi ya wafanyakazi kuwa 'chawa' wa kiongozi fulani ndani ya shirika.

Alisema hata kama serikali itawekeza fedha nyingi ndani ya shirika hilo, kama wafanyakazi wako kwenye makundi, fedha hizo zitapotea.

Pia alikemea rushwa ndani ya shirika hilo na kuwataka watumishi kujenga utamaduni wa kuwaambia wateja ukweli kuhusu muda wa kuunganishiwa umeme baada ya kulipia.

Awali, Mramba alisema watumishi wa wizara hiyo wana ari na shauku ya kufanya naye kazi ili kufikia malengo yaliyowekwa.

Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Chande, alisema menejimenti na wafanyakazi wako tayari kutekeleza maelekezo yote ili wananchi wengi zaidi wapate umeme.



Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kigoma (KUWASA), Poas Kilangi (nyuma), na mafundi bomba, Hassan Sadick (kulia) na Reani Kupela waking'oa mabomba ambayo wananchi wamejiunganishia bila kufuata utaratibu, mjini Kigoma juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanasiasa waafikiana mambo 15 ya kufuata

**Na Halfani Chusi**

VYAMA vya siasa vimeafikiana mambo 15 ya kufanya huku vikipigilia msumari kuhusu Tume Huru ya Uchaguzi, Katiba mpya, rushwa kipindi cha uchaguzi na utumiaji wa lugha za matusi kwenye mikutano ya siasa.

Hayo yamo katika maazimio yao 15 viliyotoa kwa serikali kupitia mkutano maalum wa baraza la vyama vya siasa na wadau wa demokrasia kutathimini utekelezaji wa mapendekezo ya kikosi kazi na hali ya siasa nchini uliofanyika kwa siku tatu na kutamatika jana jijini Dar es Salaam.

Maazimio mengine ni muswada wa sheria mpya ya uchaguzi, marekebisho ya sheria ya vyama vya siasa na gharama za uchaguzi uwasilishwe katika bunge la Novemba, mwaka huu, kwa hati ya dharula, kuwapo na demokrasia ndani ya vyama vya siasa kwa kuwapatia nafasi wagombea wa viti maalum ndani ya chama.

Pia vyama hivyo vimeazimia utoaji wa elimu ya R nne za Rais Samia, ili watu walielewe kusudio la serikali, vyama vya siasa viweke mkakati wa kuongeza wanawake na vijana katika siasa na uongozi.

Aidha, imeazimiwa kuwa viongozi wa dini na nyumba za ibada zisitumike kisiasa, Jeshi la Polisi lifanye kazi kwa weledi kwa kuzingatia sheria za nchi wakati wa kusimamia uchaguzi pamoja na kuweka msisitizo kwa wazazi kusimamia maadili katika familia ili kupata viongozi waadilifu.

**KAULI YA MWINYI**

Akizungumza kwa niaba ya Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, alisema serikali zote za Muungano na ile ya Zanzibar zimeyapokea maazimio hayo na kuahidi kuyafanyia kazi.

Alisema jukumu la kulinda amani ni jukumu la Watanzania wote na wakiwa viongozi, watatimiza wajibu wao ili kuepuka matendo yanayoweza kusababisha kuvunjika kwa amani.

"Amani tuliyo nayo ni tunu adhimu, hatuna budi kuilinda kwa namna yoyote kuzingatia sheria na kanuni wakati wa kufanya mikutano ya hadhara. Tusipofanya hivyo jambo hilo linaweza kusababisha vurugu.

"Tutumie matokeo ya mkutano huu kubadili tabia na kuweka uzalendo wa taifa letu mbele kuliko kitu chochote. Vijana wa sasa na vizazi vijavyo wanategemea maandalizi yetu ili waige, hivyo hatuna budi kufanya matendo mema," alisisitiza.

Pia aliwataka viongozi wa vyama vya siasa kufuata kile walichoadhimia kwenye mkutano huo kwa ajili ya kuendeleza umoja na mshikamano katika taifa.

"Tukiondoka hapa, haya ambayo tumeyazungumza tusije tukayasahau. Kila wakati tuyazungumze yawe msingi wa maisha yetu," alisema.

# Ajira 2,500 zaja makaa ya mawe Mchuchuma

**Na Beatrice Moses**

MRADI wa uchimbaji wa makaa ya mawe Mchuchuma unatarajiwa kutoa ajira rasmi 500, ajira za muda 2,000 kati ya kampuni tano za wazawa zilizotia saini mikataba ya utekelezaji.

Vilevile, serikali imebainisha kuwa wananchi 1,117 kati ya 1,142 tayari wamelipwa fidia kupisha utekelezaji wa mradi huo huku 25 hawajajitokeza kujaza nyaraka za malipo.

Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji, aliyasema hayo juzi Dar es Salaam wakati wa hafla ya utiaji saini mikataba ya mradi huo ulioko Ludewa, mkoani Njombe.

"Mradi huu una faida nyingi zikijumuisha kuingiza mapato kwa serikali na kutoa ajira 500 za moja kwa moja na 2,000 zisizokuwa za moja kwa moja," alisema.

Waziri huyo alisema Sh. bilioni 15.4 zilitengwa kwa ajili ya wanufaika 1,142. Kwa wanufaika ambao hawajajitokeza kujaza fomu, uongozi wa Wilaya ya Ludewa unawasiliana nao ili wakamilishe taratibu husika na kulipwa stahiki zao.

Waziri alisema kufanikiwa mchakato wa kuanza kwa mradi huo ni hatua ya serikali ya kuhakikisha inawanufaisha wananchi kwa kuwaondoa kwenye mkwamo uliosababishwa na kutochimbwa makaa hayo kwa miaka mingi.

Mkurugenzi Mwendeshaji wa Shirika la Maendeleo (NDC), Dk. Nicolaus Shombe, alisema awali mchakato wa kupata kampuni za wazawa kwa ajili ya mradi huo ulihusisha kampuni 25. Kati yake, 17 ziliwasilisha rasmi maombi. Baada ya mchujo zikapatikana tano.

Kampuni zilizotia saini mkataba wa makubaliano ya miaka mitano ya uchimbaji wa makaa ya mawe katika mradi huo ni Sheby Mix investment Company Limited, Nipo Afrika Engineering Company Limited, Chusa Mining Company Limited, Kindaini Company Limited na Cleveland Mine and Service Company Limited.

Dk. Shombe alisema eneo la mradi lina ukubwa wa kilomita za mraba 166. Shirika limeandaa vitalu 10 vitakavyokodishwa kwa kampuni. NDC inatarajia kila moja itachimba tani 30,000 kwa mwezi.

## HABARI KITAIFA

# Ung'oaji meno kienyeji, makofi shavuni chanzo cha usikivu hafifu



Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la kimataifa la misaada na maendeleo la Catholic Relief Services (CRS), Kellie Hyanes (kulia), akizungumza katika mkutano uliowakutanisha wadau mbalimbali jijini Dar es Salaam jana, kujadili mifumo endelevu ya usambazaji maji vijijini katika kuadhimisha miaka 60 ya utoaji huduma wa shirika hilo hapa nchini. **PICHA: JUMANNE JUMA**

**Na Renatha Msungu,**

DODOMA

UNG'OAJI meno hasa magego holela, kupigwa makofi sehemu ya mashavu na kichwani, kumetajwa kuwa chanzo cha tatizo la usikivu hafifu kwa watoto.

Mtaalamu wa Usikivu kutoka Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Kati ya Benjamin Mkapa, Dk. Leonard Tibihika, alibainisha hayo jana jijini hapa alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu tatizo hilo hususani kwa watoto.

Alisema ung'oaji hovyo wa magego na vipigo vinavyotolewa na wazazi na walimu kwa watoto hasa makofi sehemu za mashavu na kichwani ni chanzo kikubwa cha tatizo hilo kutokana na kuathiri mishipa ya fahamu.

"Kuna mishipa ya fahamu inayopeleka taarifa kwenye ubongo, hivyo inapoathiriwa kutokana na ung'olewaji hovyo magego au vipigo vya kwenye mashavu na kichwani husababisha ugonjwa na matatizo kwenye usikivu," alisema.

Pia alisema mtu anapopigwa makofi au ngumi, mgandamizo unaotokana na kitendo hicho huathiri mishipa ya fahamu inayosaidia kutuma taarifa za usikivu kwenye ubongo.

"Baadhi ya wagonjwa wanaofika kufanyiwa uchunguzi katika kitengo chetu wameonyesha vipigo ni chanzo cha watu hao kupoteza usikivu," alisema.

Tibihika alitaja sababu nyingine ni tabia ya kusafisha masikio kwa njia zisizo za kitaalamu kama vile kutumia pamba, njiti za viberiti, manyoya ya ndege, tishu, vitambaa na hata funguo.

Kwa mujibu wa mtaalamu huyo, sikio hujisafisha na kutoa uchafu hadi nje na matumizi ya vifaa kusafisha sikio si sahihi kwa sababu husukuma uchafu ndani badala ya kuutoa nje, huku chembechembe za vifaa hivyo zikisalia ndani huziba sikio.

Alisema Kitengo cha usikivu na uwekaji wa vifaa vya usikivu katika hospitali hiyo kina vifaa vya kisasa na wataalamu waliobobea katika kutoa huduma za uchunguzi na matibabu ya usikivu.

Aliitaka jamii kuwa makini na suala zima la ung'oaji meno hayo na kuwashauri kwenda kwa wataalam sahihi ili kupata tiba stahiki huku akiwataka wazazi kuepuka vipigo vinavyochangia tatizo hilo.

Dk. Joshua Yeuze, ambaye ni daktari bingwa wa magonjwa ya macho katika hospitali hiyo, alisema matatizo ya macho husababisha tatizo la usikivu hafifu na hutibika.

Alisema wagonjwa wa macho wenye matatizo ya usikivu mara nyingi wanakuwa na upungufu wa madini kama vile vitamin B12, Vitamini D na madini chuma na mara nyingi wanawapa virutubisho vya madini hayo ili kurejesha usikivu wao.

# Waziri Chana ashauri mbinu kukwepa migogoro kimkataba

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Sheria na Katiba, Pindi Chana, amezitaka serikali za mitaa na halmashauri kupata ushauri wa kisheria kutoka ofisi ya wakili mkuu wa serikali kabla ya kuingia mikataba, ili kuinusuru serikali kuingia hasara ya kulipa mamilioni ya fedha na migogoro.

Chana alitoa rai hiyo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na wafanyakazi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali alipokwenda kuwatembelea baada ya kuteuliwa na Rais Samia Suluhu Hassan kushika wadhifa huo.

Alisema taasisi za serikali, ofisi za serikali za mitaa na halmashauri nchini, zinatakiwa kuitumia ofisi hiyo kabla na wakati wa kuingia mikataba, kwa kuwa kufanya hivyo, pia kutasaidia kuepuka migogoro ambayo imekuwa ikiibuka mara kwa mara na kuisababishia hasara ya mamilioni ya fedha.

"Tunapotetea serikali zile fedha zinasaidia kuleta maendeleo na kujenga miundombinu...Wizara ya Sheria na Katiba inaacha milango wazi kwa wananchi kupata ushauri kwenye masuala ya mirathi na madai," alisema na kusisitiza kuwa: Masuala ya haki, utawala bora ndiyo msingi wa uongozi, unapokuwa na jambo lako tuambiane na serikali, vinginevyo uko mbele utakwama".

Pamoja na mambo mengine, alipongeza ofisi hiyo kwa kuitetea serikali ndani na nje ya nchi na kuokoa mamilioni ya fedha ambazo zingelipwa kama ilivyoshtakiwa. "Mmelinda nchi, haki, mmeitetea serikali ndani na nje ya nchi hongereni kwa kuokoa fedha nyingi ambazo zitatumika kujenga miundombinu na kutekeleza miradi ya maendeleo."

Vilevile, aliishauri ofisi hiyo kujenga jengo lake jirani na Mahakama Kuu Dodoma na mikoa mingine nchini, ili huduma zake ziwafikie wananchi kwa urahisi zaidi.

Awali, Wakili Mkuu, Boniface Luhende, alisema ofisi hiyo ilianzishwa ili kuimarisha uwezo wa serikali kuendesha mashauri na madai yanayofunguliwa dhidi yake.

Lubeje alitataja baadhi ya kesi ambazo ofisi yake imefanikiwa kuzimaliza na kuinusuru serikali kulipa mamilioni ya fedha kuwa ni ya ujenzi wa SGR iliyofunguliwa nchini Rwanda.

Nyingine ni ya madini iliyofunguliwa jijini London nchini Uingereza ambayo iimalizika kwa njia ya usuluhishi baada ya kuondolewa mahakamani. Kwa mujibu wa Wakili Mkuu huyo, Serikali ilitakiwa kulipa dola bilioni 3 ambazo ni sawa na Shilingi trilioni saba.

"Dola bilioni tatu sawa na Shilingi trilioni saba tumeokoa, London tumeendesha wenyewe, tungetumia kampuni tungelipa fedha nyingi mno," alisema.

Alitaja baadhi ya changamoto wanazokumbana nazo kuwa ni taasisi za umma kutokana na kutozingatia mwongozo na kusababisha mgogoro.

Vilevile, alisema kuna taasisi za serikali zimekuwa zikivunja mikataba bila kushirikisha ofisi yake na kusababisha miradi ya ujenzi kukwama.

Alisema taasisi hizo pia zimekuwa zikichelewesha malipo na kusababisha serikali kushtakiwa na kuingia katika migogoro.




**RIPOTI YA UCHUNGUZI**

## MIKOPO ASILIMIA 10

# Wakopaji waanika ulaji vigogo h'shauri

• Vumbi na jua lake, ujasiriamali unadoda...



Wajasiriamali wakiwajibika kwenye harakati zao mkoani Dar es Salaam. Kuinuka kwao kupiga hatua zaidi kibiashara, kuna unasaba wa karibu na mikopo. **PICHA: MAKTABA**

**Na Mwandishi Wetu**

NI saa 11 jioni, Mwajabu Ally, akiwa na mwanawe mwenye umri wa miaka minne, anapanga mafungu ya nyanya, vitunguu na nyanya chungu katika eneo lenye vumbi pembeni mwa barabara kuu ya Dar es Salaam -Lindi huko Mbagala Rangi Tatu, wilayani Temeke, mkoani Dar es Salaam.

Ili kujikinga na jua katika kituo hicho cha ujasiriamali, Mwajabu ana mwamvuli chakavu sawa na ilivyo kwa jirani yake, Asha Juma mwenye bidhaa kama za Mwajabu, ambazo kwa makadirio zina mtaji usiozidi Sh. 20,000.

Hizo ndizo ngome zao, kama ilivyo kwa kundi lingine kubwa la wajasiriamali wa namna hiyo, wakipambana kupata kipato kinachoendesha uhai wao na familia zao kila siku.

Kimsingi, hao wanaangukia kundi la wajasiriamali wenye kipato cha chini kabisa, mkono kwenda kinywani kunatokana na kuripoti mahali hapo kuwajibika.

Mwajabu na Asha, wote wana umri wa makamo, katika mihangaiko yao ya kujikwamua kiuchumi kutoka ngazi waliyoko, wameshawahi kuomba mikopo inayotolewa na halmashauri kwao kinamama, vijana na wenye ulemavu, fedha zitokanazo na asilimia 10 ya mapato ya ndani ya halmashauri.

Kwa mujibu wa sheria inayowezesha mikopo hiyo, mgawanyo wake ni kutoka jumla ya asilimia 10 ya mapato ya halmashauri, vijana na wanawake kila kundi linapatiwa asilimia nne huku wenye ulemavu wakipatiwa asilimia mbili.

Hata hivyo, kuna malalamiko ya kutokuwapo usawa katika upatikanaji wa mikopo kwa walengwa.

"Ninakumbuka mwaka 2019 tulitembelewa na kiongozi wa mtaa wetu, akatuambia tuunde vikundi tutapewa mikopo. Tuliunda kikundi cha wanawake wajasiriamali 10, tukachagua mwenyekiti wetu, akafuatilia lakini hadi sasa hakuna matumaini yoyote," Asha analalamika.

Anaendelea kusimulia: "Mwenyekiti alitujulisha kuwa alifuatilia sana Halmashauri ya Manispaa ya Temeke, lakini ni usumbufu tu, maana hakuna jibu la kueleweka.

"Tulikata tamaa na kusambaratika. Sasa tunaishi kwa mikopo inayotuumiza ambayo ni kausha damu. Ni mikopo umiza ambayo riba yake ni kubwa na wakati mwingine tunaweka rehani vitu vyetu vya ndani."

Mwajabu ana malalamiko kama ya jirani yake huyo, akisema: "Alikuja diwani wetu, akatwambia tuweke vikundi. Kuna mikopo ya wajasiriamali, tukaandikisha majina, tukachagua mwenyekiti alifuatilia lakini hakufanikiwa, tunaona ni usumbufu na ahadi hewa."

Mjasiriamali mwingine Mwanaidi Juma anasema alifuatwa na kiongozi mmoja eneo la soko lao akamwambia 'wewe ni mpambanaji sana wa siku nyingi. Kuna mikopo ya asilimia 10, inatolewa na halmashauri, nitafanya mpango na wewe uingie katika kikundi'.

"Wanatudanganya sana hawa watu, hakuna mikopo kwa ajili ya wafanyabiashara wala nini, wanaopewa ni wale wanaojuana, inategemea unamjua nani na uwe na fedha ya kuhonga ili uingizwe kupata hiyo mikopo. Kama mimi hapa niwe na rafiki zangu ninawatafuta ninawapa, lakini kusema kila mjasiriamali amepata mikopo hiyo ni uongo," anadai Mwanaidi.

"Wanatafutana makundi wanavyojuana wenyewe, nimeona wameingia kwenye kikundi wanatengeneza sabuni na mkaa, wana mashine za kushona, lakini sisi tunaokaa huku barabarani, sisi tunaomba neema ya Mungu, hatufikiwi. Serikali iweke utaratibu mzuri ili tupate mikopo,"anadai Elizabeth Mpangi, mkazi wa Mbagala Mission ambaye pia ni mjasiriamali.

"Mimi nipo hapa tangu mwaka 2016, ninauza bidhaa zangu hapa. Tulianza kwenye madeli tukaja kwenye majokofu na sasa wanawake wameongezeka, lakini fedha za Rais, sijui halmashauri sisi tunasikia tu, mara kuna mikopo ya bajaj, pikipiki lakini sina mwalimu wa kuniongoza kuipata," analalamika.

Mama huyo wa watoto wanne anasema ni muhimu serikali ikaja na utaratibu mzuri wa kutoa mikopo hiyo ili kuwafikia wajasiriamali halisi ambao wako sokoni na barabarani.

"Mwanangu alikuwa anasoma Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), ila ameishia mwaka wa pili baada ya kukosa ada ya Sh. 800,000 kwa mwaka. Mimi ni mama mpiganaji, nimesomesha watoto wangu mwenyewe, mwaka wa kwanza nililipa Sh. milioni 1.2, ila sasa yuko nyumbani nimeshindwa.

"Biashara hii ya maji na vinywaji baridi ndio inanisaidia, ningepata mikopo kama hiyo ingebadilisha maisha yangu, lakini wanaopata ni wajasiriamali wa kati na juu.

"Ninatamani viongozi kama wanataka kutusaidia wanawake, waje maeneo yetu ya biashara watueleze, lakini wakiwaachia viongozi wetu wa serikali za mitaa, wanapeana mikopo wao kwa wao," Elizabeth anadai.

Anabainisha kuwa wapo baadhi ya wanawake waliopata mikopo hiyo. Wanauza sabuni, lakini wale wa chini kabisa kama yeye hawana mtu wa kuwasaidia kuipata na ndio maana wako barabarani.

"Ninatamani sana kupata hizo fedha za Rais za kutuinua wajasiriamali, lakini haziwezi kunifikia kwa sababu sina 'connection' (kiungo)," anasema.

Mjasiriamali huyo anasema wangepata mikopo hiyo, wangefanya biashara katika maeneo rasmi na kulipa kodi, lakini wanalazimika kufanya biashara kando ya barabara ambako wanakutana na madhila mengi, yakijumuisha vumbi, jua na hata kuhatarisha maisha yao kwa ajali za magari barabarani.

"Wajasiriamali wadogo tupo wengi sana, lakini tunaishi maisha ya wasiwasi. Mara leo mmefukuzwa mara leo kaeni, mara mgambo hao unakaa wiki hufanyi biashara.

"Mimi nina watoto wanne; wawili wanajitegemea na wawili wananitegemea kwa kila kitu. Siwezi kulala nyumbani, lazima utoke ukatafute. Ni muhimu serikali iweke utaratibu mzuri, mikopo itufikie watu halisi ambao tunahitaji kubadilisha maisha yetu," anasema.

Neema John, mjasiriamali anayeuza mboga katika Soko la Tegeta kwa Ndevu, wilayani Kinondoni, anasema anatamani kupata mikopo hiyo, lakini "usumbufu na kujuana kumekuwa kwingi".

Anasema amesikia kuna mikopo inayoitwa ya Mama Samia. Amefuatilia katika eneo lake, hajafanikiwa kupata, hivyo anashauri serikali iweke utaratibu mzuri wa utoaji mikopo kwao.

Mwajabu Ramji, mkazi wa Mabwepande, wilayani Kinondoni, anasema alianza mchakato wa kupata mikopo hiyo kwa kujiunga katika kikundi na wenzake watano ambao walichagua shughuli za ushonaji, lakini mchakato wa kuunda kikundi ulikuwa mgumu. Akaishia njiani.

"Tuliona jirani yetu aliungana na wenzake wakapewa Sh. milioni 70. Wakafungua eneo la kufyatua matofali. Nilimwuliza akasema anafahamiana na diwani, hivyo alimsaidia kurahisisha mchakato, akapata mkopo.

"Nilichoona kwa wenzangu, anayenufaika ni mmoja tu ambaye ndiye kiongozi na wale wengine hata hatuoni mabadiliko yoyote ya maisha yao kiuchumi. Sasa ninajiuliza 'hii mikopo inasaidia kweli?'" anasema.

Rashidi Jumaa, mkazi wa Mbezi wilayani Ubungo, anasema aliungana na vijana wenzake wanne, wakaanzisha ofisi ya kuchomelea vyuma, na walifanikiwa kupata mkopo kutoka halmashauri kutokana na mzazi wa mmoja wao kuwa na urafiki na diwani.

"Diwani (hakumtaja jina) alitupeleka kwa Ofisa Maendeleo, akatembelee eneo letu. Ili upate mkopo, lazima uwasilishe maombi wayasome halafu wakutembelee na kurudisha taarifa.

"Sisi ilikuwa rahisi kwa kuwa diwani aliongea na Ofisa Maendeleo ya Jamii kisha akapitisha wazo letu, tukapata mikopo," anadai.

Rashidi anasema baada ya kupewa mkopo, walianza kurejesha baada ya miezi mitatu; Sh. 400,000 kwa mwezi na wataendelea kurejesha kwa miaka mwili hadi kumaliza.

"Ni mikopo mzuri na nafuu sana. Shida ni utartibu wake, ilitokea bahati nina mtu ninafahamiana naye, lakini kwa ambaye hana, ni vigumu sana kwa kuwa lazima uwe na fedha ya kutoa kuanzia kwa diwani na Ofisa Maendeleo ya Jamii, na unapopata mradi unapaswa kuwagawia kiasi fulani, hii siyo rahisi sana.

"Ninashauri serikali iweke utaratibu mzuri kuondoa ujanjaujanja uliopo na isiwe unapata mkopo kutokana na unayefahamiana naye, bali kwa sifa ya mradi husika.

"Kwa mfano, sasa tunapata kero, wanapiga simu kila mara, lakini pia wanatutembelea kila mara na wakija, huwezi kuwaacha bila chochote," anadai.

***ITAENDELEA KESHO**

# Uamuzi kesi kifo cha mahabusu anayedaiwa kujinyonga waiva

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kivukoni, Kinondoni, Dar es Salaam inatarajia Septemba 21 mwaka huu kutoa uamuzi wa uchunguzi wa chanzo cha kifo cha Stella Moses, aliyedaiwa kujinyonga akiwa mahabusu ya Kituo cha Polisi Mburahati alikokwenda kujisalimisha.

Uamuzi huo ulitakiwa kutolewa juzi na Mahakama ya Korona Kinondoni na Hakimu Mkazi Jacqueline Rugemalila, lakini ilishindikana kwa kuwa uamuzi haujakamilika.

"Shauri lilipangwa kwa uamuzi, bado haujakamilika. Ninaomba niwapangie tarehe, lakini ninatamani niwapangie kwa tarehe ya karibu, lakini sijui ninyi mawakili kwa nafasi yenu," alisema Rugemalila.

Baada ya hakimu kusema hivyo, Wakili wa Serikali Mwandamizi Job Mrema, alidai kuwa kwa tarehe yoyote itakayopangwa na mahakama kwa upande wao ni sawa.

Hakimu Rugemalila aliahirisha kesi hiyo hadi Septemba 21 mwaka huu kwa ajili ya uamuzi wa maombi ya kufanyika uchunguzi wa chanzo cha kifo hicho.

Awali, wajibu maombi ambao ni Mkuu wa Jeshi la Polisi na wenzake waliiomba mahakama isifanye uchunguzi huo hadi pale maombi waliyoyawasilisha yatakaposikilizwa na kutolewa uamuzi.

Wakili Mrema alidai kuwa anafahamu kwamba mahakama ilitoa amri kuhusu kufanyika uchunguzi, lakini wanaomba kusikilizwa kwa shauri hilo jipya kwanza ndipo utekelezaji wa amri yake ufuate.

Hata hivyo, Wakili Peter Madeleka aliomba mahakama kutupilia mbali pingamizi hilo kwa madai halina mashiko na linalenga kuipotezea mahakama muda wake na kwamba upande wa serikali haukutaja kifungu cha sheria ambacho kimekiukwa kwa kuwapo shauri hilo mahakamani.

Alidai maombi yaliyowasilishwa mahakamani yameletwa kinyume cha sheria kifungu cha 4, 12 cha Sheria ya Uchunguzi wa Kifo na kwamba kama shauri hilo linakiuka Katiba.

Akijibu hoja hiyo, Wakili Mrema alidai sheria haiwazuii kuleta pingamizi na kwamba wana uwezo wa kuwasilisha pingamizi hata kama kesi inakaribia kutolewa hukumu.

"Ninakubaliana na hakimu kwamba shauri hili limesikilizwa na kukamilika na amri iliyoombwa imesikilizwa na ndio maana amri imetoka. Lakini kwa kuwa uchunguzi haujafanyika, tunasisitiza kilichoombwa ni amri ya kufanya uchunguzi na kwa mujibu wa maombi yetu ipokee kama mambo ya kufikirika ambayo yamewasilishwa," alidai Mrema.

Baada ya mahakama kusikiliza hoja za pande zote, ilikubaliana na hoja za upande wa Jamhuri na kuanza kusikiliza shauri hilo kwa kumwita kutoa ushahidi aliyekuwa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kinondoni, Ramadhani Kingai na aliyekuwa Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Lazaro Mambosasa.

Inadaiwa Stella alifariki dunia usiku wa Desemba 20, 2020, akiwa mahabusu ya Kituo cha Polisi Mburahati alikojisalimisha baada ya kupata taarifa kuwa alikuwa anahitajika polisi. Alidaiwa kujinyonga akiwa mahabusu.

Wanafamilia hawakukubaliana na madai hayo. Wakaomba ufanyike uchunguzi huru kujiridhisha chanzo cha kifo cha ndugu yao wakati Jeshi la Polisi likishinikiza mwili wa marehemu uzikwe.

Shauri hilo lilifunguliwa na shemeji wa marehemu, Emmanuel Kagongo, kwa niaba ya familia ya marehemu dhidi ya Mkuu wa Jeshi la Polisi, Kamanda wa Polisi Kanda Maalum Dar es Salaam, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kipolisi Kinondoni, Mkuu wa Polisi Wilaya ya Kipolisi Mburahati, Mkurugenzi Mkuu wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

## Ukosefu elimu chanzo wimbi usafirishaji nyara za serikali

**Na Jenifer Gilla**

WADAU wa usafirishaji wa majini nchini wamesema ukosefu wa elimu ya utambuzi wa mizigo yenye nyara za serikali ni chanzo kikuu cha kupakia mizigo hiyo na kuisafirisha nje ya nchi.

Waliyasema hayo juzi jijini Dar es Salaam wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya kutambua mizigo yenye nyara za wanyamapori kwa wadau wa usafirishaji wa majini, yaliyotolewa na Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID) kupitia Mradi wa Tuhifadhi Maliasili.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi za Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), John Ulanga, alisema wakati mwingine wamekuwa wakiipakia mizigo hiyo na kuisafirisha kwa kutumia vyombo vyao vya usafiri bila kujua.

Alisema baada ya mafunzo hayo, anatarajia kupata mbinu na mikakati ya kutambua mizigo iliyoficha nyara hizo zinazosafirishwa kinyume cha sheria, hivyo kuwa mjumbe namba moja wa kutokomeza biashara hiyo.

Kwa mujibu wa Ulanga, kumekuwa na matukio mbalimbali ya kimataifa ya usafirishaji haramu wanyamapori ikiwamo wa Tanzania hali inayoleta hasara katika sekta ya utalii nchini kwa kuwa ndiyo sekta inayoongeza kuleta fedha za kigeni.

Katibu Mtendaji wa Baraza la Wasafirishaji Shehena Tanzania, Sallu Johnson, alisema elimu atakayoipata atakwenda kuitoa kwa wasafirishaji wenzake katika maeneo yote nchini ili kuongeza kasi ya udhibiti wa biashara hiyo ambayo imekuwa tatizo kubwa duniani.

Kaimu Mkurugenzi Msaidizi wa Uzuiaji Ujangili kutoka Wizara ya Maliasili na Utalii, Kiza Baraga, alisema sekta binafsi ina mchango mkubwa katika kuhifadhi maliasili iwapo itapewa elimu ya utambuzi.



Balozi wa Saudi Arabia nchini, Yahya Ahmed Okeish, akizungumza kwenye mkutano na waandishi wa habari uliowakutanisha madaktari bingwa wa moyo kutoka Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI), jijini Dar es Salaam jana, akiwasilisha salamu za Mfalme Salman wa nchi hiyo, aliyedhamini kambi ya upasuaji wa moyo kwa watoto 30 wenye matatizo ya moyo nchini. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

# Watoto 500 wasubiri upasuaji wa moyo JKCI

**Na Christina Mwakangale**

WATOTO 500 wenye matatizo ya moyo wanasubiri kufanyiwa upasuaji wa moyo katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI).

Wakati hao wakiwa katika foleni kupata huduma hiyo, wengine 30 wamefanyiwa upasuaji katika kambi maalumu ya matibabu iliyoanza Septemba 9, mwaka huu katika taasisi hiyo.

Kambi hiyo inahitimishwa leo, upasuaji kwa watoto hao umefanywa na mabingwa wa upasuaji wa moyo kutoka JKCI kwa kushirikiana na wenzao wa Kituo cha Mfalme Salman cha Misaada ya Kibinadamu cha Saudi Arabia.

Mkurugenzi Mtendaji wa JKCI, Dk. Peter Kisenge, akizungumza jana Dar es Salaam baada ya Balozi wa Saudi Arabia nchini, Yahya Ahmed Okeish, kutembelea taasisi hiyo kwa lengo kuwashukuru mabingwa hao na kufikisha salamu za Mfalme Salman wa Saudi Arabia, alisema nchi hiyo imefadhili kambi ya upasuaji wa moyo kwa watoto 30.

Alisema mabingwa hao kutoka Saudi Arabia tangu wameanza kutoa huduma kwa ushirikiano mwaka 2019, wameshahudumia wagonjwa 439 kupitia kambi tofauti katika taasisi hiyo na kuokoa takribani Sh. bilioni 3.5 iwapo matibabu hayo yangefanyika nje ya nchi.

"Mwaka 2019 wenzetu wa Saudi Arabia waliwafanyia upasuaji wagonjwa 100 na wakarudi tena mwaka 2022 na kuwahudumia wagonjwa 60. Hii inatokana na undugu tulionao kati ya Tanzania na Saudi Arabia. Kambi hii ya sasa ambayo inahudumia wagonjwa 30, tumeokoa fedha nyingi ambazo zingetumika nje ya nchi iwapo wangetibiwa huko.

"Watoto wengi wana tatizo na ni kubwa na wengi hupoteza maisha kwa kukosa matibabu, upasuaji wa moyo. Takwimu zinaonesha katika kila watoto 1,000 wanaozaliwa mmoja ana tatizo la moyo," alisema Dk. Kisenge.

Pia alibainisha kuwa uwapo wa kambi hiyo na wenzao kunawasaidia kuwaimarisha wataalamu wa Kitanzania na wanaotoka nchi jirani ambao hufika JKCI kwa ajili ya kujifunza utoaji matibabu ya kibingwa ya moyo.

Mkuu wa Kitengo cha Upasuaji kwa Watoto kutoka taasisi hiyo, Dk. Angela Muhozya, alisema nchi hizo mbili zimekuwa zikishirikiana tangu JKCI, ikiwa change hadi sasa ilipoongeza wigo wa matibabu ya kibingwa kwa ukanda wa Afrika Mashariki.

"Watoto wanaoaubiri foleni ya upasuaji wanafikia 500 hivyo mtaona kuwapo kwa mpango huu wa ushirikiano na wenzetu nchi tofauti, inasaidia kupunguza idadi kubwa ya mahitaji ya watoto kupata matibabu ya moyo hapa nchini ambao idsdi yao ni kubwa," alisema bingwa huyo.

Kaimu Mkurugenzi Idara ya Mashariki ya Kati kutoka Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Leonce Bilauri, alisema ushirikiano kati ya nchi hizo mbili, unaendelea kukua hususan kwenye miundombinu, elimu na afya.

Janet Njimba, mama wa mtoto Jamal Tikiti (9), amabye amefanyiwa upasuaji kwenye kambi hiyo, aliishukuru serikali pamoja na nchi hiyo kwa kuwapatia huduma ya upasuaji watoto wao.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Bodi mpya ya TRA itekeleze ipasavyo maagizo ya Mbarawa

**WAZIRI** wa Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, juzi alizindua bodi mpya ya wakurugenzi ya Shirika la Reli Tanzania (TRC) huku akibainisha kutoridhishwa na uendeshaji wa taasisi hiyo kongwe katika sekta ya uchukuzi. Sababu kubwa, kwa mujibu wa Prof. Mbarawa ni kushindwa kufikia malengo yaliyowekwa.

Katika hafla hiyo iliyofanyika jijini Dar es Salaam, Waziri Mbarawa alisema hivi sasa TRC inajenga miundombinu ya reli ili kupanua wigo wa usafirishaji mizigo lakini kiuendeshaji haifanyi vizuri.

Alitolea mfano wa kuwapo mikataba kati ya wizara na bodi iliyopita kuhusu uendeshaji lakini hakuna kilichofanyika. Pia alisema suala la tiketi mtandao nalo limekuwa likisuasua hali inayoonyesha matundu ya utendaji mbovu ndani ya taasisi.

Sambamba na hilo, alisema Kigoma kuna watu walimelipa kusafirishiwa saruji lakini hakuna hata shehena inayokwenda na kwamba pamoja na kupiga simu hakuna kinachofanyika. Kwa mujibu wa Waziri, kama shirika lingesafirisha shehena hiyo, ilitarajiwa bei ingekuwa rahisi na kurahisisha kazi mbalimbali lakini kinyume chake makandarasi wamesimamisha kazi kwa kukosa bidhaa hiyo.

Kutokana na mwenendo huo, Mbarawa aliagiza bodi mpya kuhakikisha utendaji ndani ya shirika hilo unabadilika na kuwa wa viwango ikiwamo kujipanga katika uendeshaji wa Reli ya Kisasa (SGR) kwa kuwa tayari serikali imepitisha sheria kuruhusu sekta binafsi kutumia reli. Katika mfumo wa sasa wa uendeshaji reli kampuni binafsi ambazo zina mabehewa zinaruhusiwa kutumia reli zilizopo kusafirisha mizigo yao au ile ya kukodisha.

Pamoja na kuhimiza kubadilika kiutendaji, Mbarawa pia alizitaka bodi na menejimenti kutangaza fursa za ajira ndani ya shirika kulingana na mahitaji lakini akasisitiza kuwa fursa hiyo isitumie mwanya wa kufanya mambo kwa upendeleo wa undugu.

Kauli hiyo ya Waziri imetolewa kwa wakati kutokana na ukweli kwamba kwa sasa TRC iko katika kasi ya utekelezaji wa ujenzi wa reli ya SGR ambayo katika baadhi ya vipande imekamilika kwa kiwango kikubwa. Kutokana na hali hiyo ni lazima kujipanga katika uendeshaji wa shirika husussan kwenye usafirishaji wa abiria na mizigo.

Reli ni aina ya usafirishaji wa abiria na mizigo wa uhakika na wenye kuaminika na hutumia gharama nafuu na kubeba bidhaa nyingi kwa wakati mmoja. Kwa mantiki hiyo kama shirika litajipanga kiutendaji, ni dhahiri kwamba itakuwa tegemeo la watu wengi katika sekta ya uchukuzi.


Kutokana na kukosekana kwa usafiri wa uhakika wa uchukuzi kupitia reli, watu wengi wamekuwa wakitumia malori na mabasi ambayo uhakika wake, kwa maana ya muda na gharama imekuwa changamoto kwa wengi. Ujio wa reli ya kisasa, mathalani, utakuwa mkombozi kwa wengi kwa kuwa unatumia muda mfupi kutoka sehemu moja kwenda nyingine.

Ushauri na maagizo yaliyotolewa na Waziri yanapaswa kufanyiwa kazi kwa vitendo. Ni imani kwamba bodi mpya inayoongozwa na mwenyekiti mbobezi katika masuala ya maendeleo ya uchumi hususan katika masuala ya usafirishaji, Watanzania wanatarajia kuwapo kwa mabadiliko kama ilivyoelekezwa.

Aidha, ni dhahiri kwamba kama bodi mpya ya TRC ambayo mbali na mwenyekiti ina magwiji katika sekta ya uchukuzi itajipanga ipasavyo na kuisimamia vyema menejimenti , Watanzania watarajie matunda chanya. Kimsingi, shirika hilo litakuwa kimbilio la wananchi katika usafiri wa abiria na usafirishaji wa mizigo na hatimaye kuchangia vyema pato la taifa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita. 0713 578284,
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

Na Ester Mbilinyi, TUDARCo

# Tuyafikie maadili kwa mjumuiko wa malezi bora, adabu, wazazi kuwajibika

**KILA** mahali unapoenda iwe nje au ndani ya nchi, msamiati malezi ni wa lazima, hauna mjadala. Ni kipaumbele cha ubinadamu na kimsingi ndio maisha yenyewe ya sasa na yajayo, kwako na wanaokutazama.

Zao la malezi bora kwa mtoto, linatajwa kuwa kichocheo cha maadili mema katika jamii, licha ya kwamba hivi sasa halipewi kipaumbele kutokana na shughuli zilizotapakaa, pia mtindo wa maisha kwa baadhi ya wazazi na walezi katika familia zao.

Baadhi ya wazazi na walezi wamejikita zaidi katika shughuli ya utafutaji maisha na kusahau jukumu lao la malezi katika familia. Kuna wazazi wamekuwa wakiwaachia jukumu la malezi 'wadada wa kazi' maarufu kama 'house girls' kitu kinachochangia wanakosa ukaribu na familia zao.

Mzazi anayefahamika kwa jina la Jane Mapunda, mkazi wa Riverside Ubungo, Dar es Salaam, ana maoni yake katika eneo hilo alieleza maoni yake, kwamba wazazi na jamii kwa ujumla, wanatakiwa washiriki katika malezi na kutenga muda maalumu, wakikaa na kuongea na familia zao.

"Wazazi wengi wamekuwa 'bize' kutafuta maisha kwa ajili ya familia, lakini watenge muda wa kukaa na kuzungumza na watoto wao kwa kuwahoji na kuwaeleza mambo mbalimbali, vilevile wazazi waache kuwapeleka watoto wao kulelewa na bibi zao, kwani akina bibi hao tayari wanakuwa wameshazeeka,' anasema.

Kadhalika mwananchi Patricki Mgao, ana mtazamo kuwa watoto wanahitaji malezi kutoka kwa wazazi wote wawili na jamii kwa ujumla, ili kuepuka changamoto zinazotokana na ukosefu wa malezi bora akitamka; "Nimeshuhudia na kusikia watoto wengi wakibakwa na kulawitiwa katika jamii, jambo ambalo linatokana na wazazi, walezi kutopata muda wa kukaa na kuongea na watoto wao na hata kufatilia mienendo na maendeleo yao".

> **Mzazi anayefahamika kwa jina la Jane Mapunda, mkazi wa Riverside Ubungo, Dar es Salaam, ana maoni yake katika eneo hilo alieleza maoni yake, kwamba wazazi na jamii kwa ujumla, wanatakiwa washiriki katika malezi na kutenga muda maalumu, wakikaa na kuongea na familia zao.**

Makamu wa Rais Dk. Philip Mipango, anazungumzia kuhusu kuporomoka kwa maadili miongoni mwa vijana wengi, hata ikasababisha wakose uadilifu, wakiishia kujiingiza katika vitendo visivyofaa kama vile matumizi ya dawa za kulevya, unyang'anyi, rushwa na utapeli.

Aidha. Dk. Mipango anasisitiza akiwataka vijana kutambua uadilifu ni mtaji wa kuaminiwa na kufanikiwa na kuwataka wazazi na walezi, viongozi wa dini na kimila, vyombo vya ulinzi na usalama, vyombo vya habari, mitandao ya kijamii na vijana wenyewe katika kujenga maadili ya vijana wa Kitanzania.

Taasisi za kidini na mashirika yanayohusika na suala la malezi, huu ni wakati na fursa sahihi kwenu mkaandaa, pia kuendeleza mifumo itakayosaidia kutoa elimu ya malezi bora, ili kupunguza wimbi la mmomonyoko wa maadili katika jamii zetu, maana ishara ya tunakoenda si nzuri kabisa.

Niwageukie enyi wazazi, mkiwa ni wadau wakuu wa jambo hili, kwamba mnatakiwa kutoa elimu na usimamizi kwa watoto wa kike wanapokaribia kukua (kuvunja ungo) na wa kiume waliofika umri wa kukomaa, ili kuepuka athari zinazoweza kuwakumba katika umri mdogo.

Hapo kwa uchache nataja madhara kama vile, vijana na dimbwi la mimba za utotoni, hata madhara ya maradhi tajwa.

Inakuwa ni mazingira ya kutatanisha kuanzia anayepatwa na shida hiyo, hadi kwa wazazi ndugu na jamaa, pia katika hatima ya kufadikia kilele cha kitaifa.

Kijana anakuwa katika hatua za kukomaa na kutegemewa kote huko, vilevile mwenyewe kujitegemea katika mwelekeo wa taifa lijalo. Wenzetu wenye maono ya kitalaamu katika dira ya kwenda mbali zaidi, husimama na dhana 'kuzuia ni bora zaidi, kuliko kusonga na hatua ya kuponya.'

Ni kwanini kijana mbichi ukajiingiza katika harufu mbaya, badala ya kujitoa kuepuka madhila hayo yote, hata tukabaki kuwa na rasilimali muhimu?

HABARI KITAIFA

# Majaliwa kuzindua huduma za pamoja wawekezaji

**Na Joseph Mwendapole**

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, anatarajiwa kuzindua mfumo wa kielektroniki wa kuhudumia wawekezaji mahala pamoja ujulikanao kama Tanzania Investment Electronic Window.

Hayo yalisemwa juzi jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi wa Idara ya Uhamasishaji Uwekezaji wa Kituo cha Uwekezaji (TIC), John Mnali, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu uzinduzi huo.

Alisema mfumo huo utakaozinduliwa Jumamosi umetokana na kuunganishwa kwa mifumo mbalimbali ya taasisi za serikali ambazo zinahusika na kutoa vibali na leseni kwa wawekezaji.

Alisema taasisi hizo zimeunganisha mifumo yao ambayo inatumika kusajili wawekezaji na kutoa vibali na kwamba kwa awamu ya kwanza mfumo huo utaunganisha taasisi saba.

Alisema mfumo huo utaunganisha Wakala wa Usajili wa Leseni na Biashara (BRELA), Mamlaka ya Mapato (TRA), TIC kwaajili ya utoaji wa leseni na vyeti vya uwekezaji, Kamishna wa Kazi kwaajili ya vibali vya kazi, Uhamiaji kwaajili ya vibali vya kazi kwa wawekezaji wageni.

Alitaja taasisi zingine zitakazounganishwa na mfumo huo kuwa ni Wakala wa Vitambulisho vya Taifa (NIDA), Wizara ya Ardhi kwaajili ya ardhi kwaajili ya kuwahudumia wawekezaji wa kigeni.

"Kwa awamu hii mwekezaji atakuwa anaingia kwenye mfumo mmoja atakapoanza usajili wa kampuni ataendelea na kuomba vibali mbalimbali kupitia mfumo huo na taarifa zake za awali ambazo mwekezaji atakuwa amezitoa kama jina lake, jina la kampuni, wamiliki wa kampuni taarifa hizo zitapatikana kwenye taasisi zote za serikali bila kulazimika kutoa taarifa hizo kila wakati," alisema Mnali.

Mnali alisema mfumo huo utamrahisishia mwekezaji kupata vibali na leseni mbalimbali ndani ya muda mfupi tofauti na ilivyokuwa kabla ya mfumo huo kwa kuwa taasisi zitakuwa pamoja.

Alisema kupitia uzinduzi huo wanatarajia pia kuzindua mwongozo utakaotumiwa na watoa huduma kwa wawekezaji kwani baadhi wawekezaji huwa wanaomba huduma ya usajili wakiwa nje ya nchi.

"Kuna wakati mwekezaji yuko nje ya nchi na anataka kusajili kampuni au kupata leseni kwa hiyo siku ya uzinduzi wa dirisha la pamoja pia tutazindua mwongozo wa watu hawa wanaotoa huduma hizi kwa wawekezaji, hii huduma tunaita Investors Service Providers Guidelines," alisema.



Mkazi wa Bungo, wilayani Kibaha mkoani Pwani, Dorice Ogiro (40), akionyesha sehemu ya majeraha aliyopata baada ya nyumba kuchomwa moto na aliyekuwa mume wake. **PICHA: JULIETH MKIRERI**

# Aliyeunguzwa moto na mtalaka wake aomba kesi yake isikilizwe

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MKAZI wa Bungo Wilaya ya Kibaha, Dorice Ogiro (40), amelalamika kuhusu ucheleweshwaji wa kesi yake kufika mahakamani ili apate haki yake baada ya kuunguzwa moto na aliyekuwa mume wake.

Dorice ambaye alikuwa mke wa Elewa Joseph, walipeana talaka na mahakama iliamuru mali walizopata pamoja ikiwamo nyumba viuzwe ili wagawane.

Hata hivyo, kabla ya utekelezaji wa agizo la mahakama, inadaiwa Elewa alifika nyumbani anakoishi Dorice na mtoto wake mwenye umri wa miaka 11 na kumwaga mafuta yanayodaiwa kuwa ya petroli kwenye chumba cha jiko na kuwasha moto.

Akizungumza na Nipashe juzi mjini Kibaha Dorice alisema Juni 23 majira ya saa mbili usiku, Elewa alifika nyumbani na kumkuta akiwa na mwanae jikoni wanakula bila kusalimia wala kuongea chochote alifungua chupa ya maji inayodhaniwa kuwa na petroli na kuanza kumwaga jikoni.

"Aliingia bila hodi alinikuta tunakula na mwanangu na alikuwapo dereva boda pembeni amesimama anasubiri hela yake baada ya kuniletea maji, alimsukuma pembeni akaendelea kumwaga mafuta alikanywa asifanye hivyo, lakini hakuongea kitu alivyomaliza kumwaga alinisogelea akanimwagia mkononi na kwenye nguo," alisema.

Inadaiwa baada ya kuwasha moto eneo alilomwaga mafuta, Dorice alipokuwa anajihami kukimbia nje alizuiwa na kijana wa mtuhumiwa ambaye alikuwa anampiga na kumsukuma ndani asitoke.

Hata hivyo, baada ya muda majirani walifika kusaidia kuzima moto huo na Elewa alivyoona tukio limeisha aliondoka nyumbani hapo na kuelekea anakoishi jijini Dar es Salaam.

Alisema alienda hospitali kwa msaada wa msamaria mwema ambaye alimpatia fedha za matibabu, kwa kuwa pamoja na kuwa mtuhumiwa alishuhudia alivyomjeruhi katika mkono wake wa kulia na mapajani, lakini hakumpatia msaada.

Kwa mujibu wa Dorice baada ya kutoa taarifa polisi wiki tatu baadaye mtuhumiwa alikamatwa na kutoka kwa dhamana.

"Nilipigiwa simu na mmoja wa askari akiniambia mume wangu anaomba tuyamalize na anatuma Sh. 100,000 baadaye ataongeza nyingine, nilikataa ombi hilo nikawaambia kesi iende mahakamani nipate haki yangu."

"Pia ndugu wa mume wangu ambaye ni shemeji alinipigia simu, alikuja Kibaha kituo cha Msikitini akiwa na mtoto wa wifi yangu naye alikuwa anaomba kesi tuimalize nisamehe isiende mahakamani jambo ambalo nililikataa," alisisitiza.

"Hadi sasa sijajua lini polisi wanakamilisha taratibu zao na kufikisha kesi mahakamani, nikienda kufuatilia naambiwa jalada liko ofisi ya mwendesha mashtaka, nikienda huko naambiwa limerudishwa polisi kwa marekebisho," alisema.

Dorice aliomba Jeshi la Polisi kufikisha kesi yake mahakamani na kwamba kwasasa anaendelea kuuguza majeraha ya moto, mkono wake ulioungua na kuteguka.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Muhudhwari Msuya, alisema suala hilo lipo ofisi ya Wakili wa Serikali na taratibu zikikamilika litafikishwa mahakamani.

## KABWELA

**Na Fadhil Mohammed**






Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji (katikati), akishuhudia utiaji saini wa mikataba ya uchimbaji makaa ya mawe kwa wachimbaji wazawa katika eneo la Mchuchuma kati ya Mkurugenzi Mtendaji wa Chusa Mining Ltd, Joseph Mwakipesile (kushoto) na Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Taifa la Maendeleo (NDC), Dk. Nicolaus Shombe (wa pili kulia), jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Mwanasheria wa NDC, Mwantumu Salim. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# CRDB yazindua 'Bima ya Buku' maalum kwa bodaboda, bajaji

**Na Mwandishi Wetu**

MKUU wa Wilaya ya Kinondoni, Saad Mtambule, imepongezwa kwa uzinduzi wa mpango nafuu wa huduma ya bima inayowalenga madereva wa pikipiki na bajaji za abiria, uliopewa jina la 'Bima ya Buku'.

Mpango huo unaotajwa kutoa fursa ya kujihakikishia ulinzi wa chombo na matibabu ya afya kwa kuanzia Sh. 1,000, utakwenda kusaidia kuchochea ujumuishi wa kibima nchini.

Alitoa pongezi hizo jana kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam wakati wa hafla ya uzinduzi wa huduma hiyo iliyofanyika viwanja vya Biafra, mkoani Dar es Salaam na kuhudhuriwa na madereva wa bodaboda na bajaji zaidi ya 5,000.

"Takwimu zinaonesha Watanzania wanaotumia huduma za bima ziko chini, hivyo niipongeze Benki ya CRDB kwa kuja na mpango huu ambao ninaamini utasaidia kuwafikia wananchi wengi hasa madereva hawa wa bodaboda na bajaji.

"Kinachowakwamisha wananchi wengi kutumia huduma za bima ni pamoja na jinsi huduma hizi zinavyopatikana ikiwamo gharama. Bima ya buku imekuja kuleta jibu katika changamoto hii, niwapongeze sana Benki ya CRDB," alisema Mtambule.

Alitoa rai kwa Benki ya CRDB na taasisi nyingine za kifedha hususani kampuni za bima, kutoa elimu ya kutosha kwa wananchi.

Alisema iwapo wananchi wataelimishwa na kuelekezwa namna ya kuipata huduma hiyo kokote waliko, idadi ya wanaoitumia huduma hiyo itapanda, hivyo kuongea tija kwa taifa.

Aliwashauri madereva bodaboda na bajaji kuchangamkia fursa hiyo ya 'Bima ya Buku' ili kujilinda na majanga yanayoweza kutokea katika shughuli zao za kutoa huduma za usafiri na kuimarisha afya zao kupitia bima ya afya ambayo imeunganishwa katika mpango huo.

Akiielezea mpango huo wa 'Bima ya buku', Ofisa Mkuu wa Biashara wa Benki ya CRDB, Boma Raballa, alisema ni bima inayomwezesha mmiliki wa bodaboda au bajaji kukilinda chombo chake pamoja na afya yake kwa gharama ya kuanzia Sh. 1,000 atakayoilipa kila siku.

"Malipo ya bima hii yatafanyika kwa miezi mitatu yaani siku 86 mpaka kumaliza kuilipia mteja kunufaika na faida za bima ndogo ya chombo chake.

"Kwa anayetaka bima ndogo na bima ya afya, atatakiwa kulipia kwa miezi 11, yaani siku 333 lakini ikitokea amepata tatizo kabla hajamaliza malipo yake, atapata huduma stahiki na ataendelea kulipia bima yake," alisema Raballa.

Alifafanua kuwa kwa kawaida, bima hulipwa kiasi chote mara moja, hivyo benki imekuja na utaratibu tofauti ili kuwawezesha wajasiriamali hao wadogo kupata kinga wanayoihitaji.

"Sokoni bima ya afya inaanzia Sh. 192,000, hivyo Benki ya CRDB imeleta njia nafuu inayomruhusu kila mmiliki wa bodaboda au bajaji kuwa na uhakika wa kukilinda chombo chake pamoja na kupata matibabu iwapo ataugua au kupata jeraha.

"Kwa kuwa na bima hii mteja anajihakikishia matibabu katika hospitali yoyote ya serikali nchini endapo atapata janga mfano kuugua ghafla au kupata ajali," alisema.

Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Bima (Bancassurance) wa Benki ya CRDB, Moureen Majaliwa, alisema kuwa tangu Machi 2021, benki hiyo imekuwa wakala wa huduma za bima, hivyo kuwa na uzoefu wa kutosha ambao unawaruhusu kubuni bidhaa mpya zitakazosaidia kukidhi mahitaji ya wateja wao sokoni.

"Kutokana na uzoefu huo, Benki ya CRDB imeona kuna haja ya kuongeza wigo wa utoaji huduma za bima ili kuwafikia wananchi wengi zaidi hasa wenye kipato cha chini ili kuyakinga maisha na mali zao," alisema.

# Madalali, wasambazaji nyaraka za mahakama wapewa angalizo

**Na Yusufu Lulungu**

JAJI wa Mahakama Kuu ambaye pia ni Jaji Mfawidhi Kituo Jumuishi cha Masuala ya Mirathi na Familia Temeke, Mwanabaraka Mnyukwa, amewataka madalali na wasambazaji nyaraka za mahakama kuwa waadilifu watakapopata na wanapotekeleza majukumu yao.

Amesema kazi hiyo inapaswa kufanya kwa uandilifu ili kuhakikisha haki inatekelezwa vyema kwa pande zote mbili; mteja wanayempatia huduma na mtoa haki ambaye ni mahakama.

Jaji Mwanabaraka alitoa rai hiyo juzi alipofungua mafunzo hayo kwa wadau hao wa mahakama katika Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo (LST), jijini Dar es Salaam.

Mafunzo hayo yanaendeshwa na Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto (IJA). Yatafikia tamati Septemba 25 mwaka huu.

Chuo cha IJA kinaendesha mafunzo haya kwa mujibu wa Kanuni ya 4 na ya 6 za Kanuni za Madalali na Wasambaza Nyaraka za Mahakama za Mwaka 2017, Tangazo la Serikali Na. 363.

"Kazi ya usambazaji nyaraka za mahakama inahitaji uadilifu wa kiwango cha juu, uadilifu kwa mteja unayemhudumia, lakini pia uadilifu kwa sisi ambao mwisho wa siku ndio tutatusaidia kwenye kutoa haki.

"Utakaposema mteja hakupatikana wakati hukumtafuta, tayari utakuwa hujatenda uadilifu na unaweza kusababisha haki isitendeke ipasavyo," alionya Jaji Mwanabaraka.

Alisema mafunzo hayo ni sehemu ya maboresho makubwa ya mahakama yanayolenga kuondoa malalamiko ya wananchi kuhusu ukosefu wa maadili kwa baadhi ya watu wanaojishughulisha na kazi hiyo ya udalali na usambazaji nyaraka za mahakama.

"Mafunzo haya ni mojawapo ya sehemu ya maboresho makubwa yanayoendelea katika Mhimili wa Mahakama kwa lengo la kuondoa malalamiko mengi yaliyokuwapo kutoka kwa wananchi hususani suala la ukosefu wa uadilifu na uelewa sahihi wakati wa utekelezaji majukumu ya udalali na usambazaji wa nyaraka za mahakama," alisema.

Mratibu wa mafunzo hayo, Nuhu Mtekele, kutoka IJA, alisema mafunzo hayo yana malengo makubwa matatu - ikiwamo kuwawezesha washiriki kuwa na weledi katika kazi hiyo na pia kuunga mkono juhudi za serikali za kuwezesha ajira.

"Mafunzo haya yana malengo makubwa matatu ikiwamo kuboresha huduma zinazotolewa na mahakama ili kuwawezesha madalali na wasambaza nyaraka za mahakama kuweza kufanya kazi hiyo kwa weledi.

"Pia, kuunga mkono juhudi za serikali za kuwezesha ajira, kwa kuwa washiriki wakitoka hapa wanakwenda kujiajiri au kuajiriwa, hivyo unakuwa ni mchango mkuwa wa IJA kuongeza wigo wa ajira nchini," alisema Mtekele.

Mratibu huyo alisema mafunzo hayo pia yanasaidia ukuaji wa sekta binafsi kwa kuwa madalali wa mahakama pia wanakuwa na sifa ya kutumika na taasisi mbalimbali kama benki katika kufanya kazi ya upigaji minada, hivyo kama benki zitahitaji kukusanya madeni, zikiwatumia watu hao ambao wamepatiwa mafunzo.

Baadhi ya washiriki wa mafunzo haya, akiwamo Boaz Ackimu kutoka kampuni ya udalali ya Isoko Auctioneers & Court Broker, walisema mafunzo hayo ni muhimu kwao kwa kuwa ni kazi nyeti inayohitaji uadilifu mkubwa.

"Kama washiriki tunategemea kujifunza maadili yanayoongoza tasnia hii ya udalali wa mahakama na usambazaji wa nyaraka za mahakama.

"Ifahamike kuwa hii ni kazi nyeti inayohitaji uadilifu mkubwa, hivyo ni muhimu kwetu kujifunza sheria na kanuni zinazoongoza tasnia hii," alisema Boaz.

Mshiriki mwingine, Aneth Ndimuhela kutoka kampuni ya Rapitech Solutions Ltd. alitaja faida zingine watakazozipata kupitia mafunzo haya, akisema:

"Yana mchango mkubwa kwetu kwa kuwa yanatusaidia kuongeza ujuzi na kuweza kufanya kazi kwa weledi na kupata sifa stahiki za kufanya kazi hii.

"Pia kama ilivyo kawaida, sisi tunatakiwa tutende haki kwa mteja aliyetupa kazi na yule tunayemwendea ndio maana tunapatiwa mafunzo haya," alibainisha Ndimuhela.



# Biteko atoa maagizo tisa kwa wadau, mashirika, taasisi

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

NAIBU Waziri Mkuu, Dk. Dotto Biteko, ametoa maagizo tisa kwa wadau wa maendeleo, mashirika ya kimataifa na taasisi zisizo za kiserikali (NGO'S), asasi za kiraia na maofisa wa umma, kuhakikisha wanafanya tathimini na ufuatiliaji wa majukumu yao ya kila siku, ili kuleta matokeo chanya kwenye utendaji kazi wa serikali.

Alitoa maagizo hayo jana jijini Arusha wakati akifungua kongamano la pili la kitaifa la wiki ya ufuatiliaji na tathimini kwa niaba ya Waziri Mkuu Kassim Majaliwa.

Dk. Biteko alitoa maagizo kwa maofisa masuuli wote kwa kuwataka kuwezesha vitengo vya ufuatiliaji na tathmini, katika wizara na taasisi zao, kwa kuhakikisha uwepo wa wataalamu wa kutosha, vitendea kazi na rasilimali fedha ili kuiwezesha utekelezaji wa majukumu kwa ufanisi.

Pia, aliwaagiza wadau wote wa maendeleo yakiwemo mashirika ya kimataifa, mashirika yasiyo ya kiserikali, asasi za kiraia, kuendelea kushirikiana na serikali katika kuhakikisha shughuli za ufuatiliaji na tathmini zinafanyika ikiwa ni pamoja na kujenga utamaduni wa kufanya ufuatiliaji na tathmini.

Dk. Biteko aliwaagiza watendaji kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu kupokea mrejesho kutoka kwa wadau waliopo pamoja na kufanyia kazi maeneo yote yenye udhaifu yatakayobainishwa pamoja na kuweka mikakati ya kuongeza bidii zaidi kwa yale maeneo ambayo wamefanya vizuri.

"Mfumo jumuishi wa ufuatiliaji na tathmini ya utendaji wa shughuli za serikali unaoandaliwa uweke kipengele cha mrejesho kwa idara na taasisi zilizofanyiwa tahmini pamoja na kutoa mrejesho wa utekelezaji wa maelekezo ya viongozi wa juu," alisema.

Vilevile, aliagiza ripoti za tathmini zifanyiwe kazi na idara husika ili maeneo yenye changamoto yawekewe mkakati wa muda mfupi na mrefu wa utatuzi.

Aidha, aliagiza kila idara iwajibike kuzifanyia kazi ripoti hizo katika muda utakaobainishwa, kufanya maandalizi ya mfumo jumuishi yaende sambamba na mkakati wa habari na mawasiliano, ili taasisi zote za serikali ziwe na uelewa wa pamoja kuhusu dhima na tija ya mfumo jumuishi wa ufuatiliaji na tathmini.

Kadhalika, aliagiza taasisi zote za umma zijifanyie tathmini ya utayari ili kubaini changamoto na fursa walizonazo, katika kutekeleza mfumo wa ufuatiliaji na tathmini na kuandaa mipango ya ufuatiliaji na tathmini katika taasisi zote za umma.

"Mnatakiwa kuitekeleza sera ya taifa ufuatiliaji na tathmini inakamilika kwa haraka ili ianze kutumika kama nyenzo muhimu ya kuongoza muelekeo wa serikali na wadau katika kutekeleza jukumu la ufuatiliaji na tathmini nchini," alisema Dk. Biteko.

Agizo lingine aliwataka kukamilisha uundaji wa mfumo jumuishi wa kielektroniki, ufuatiliaji na tathimini ya utekelezaji wa mipango, programu na miradi ili kuwezesha mifumo ya utendaji kazi kusomana.

Alisema anaamini malengo ya kongamano hilo litaleta tija kwa serikali kwani litawajengea utayari, uelewa na kujiamini katika kutekeleza majukumu ya ufauatiliaji na tathmini.

Hata hivyo alitoa wito wa kufanya maboresho yatakayoweka misingi madhubuti ya ufuatiliaji na tathmini ya shughuli za serikali lakini pia ni utekelezaji wa maelekezo ya ilani ya uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020 kwa serikali.



Meneja wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) Kanda ya Kaskazini, Lorivu Lon'gidu (katikati), akizungumza na wafanyabiashara binafsi wa mafuta kutoka kanda hiyo, katika kikao kazi chenye lengo la kuwakumbusha wajibu wao na taratibu za uuzaji wa bidhaa hiyo, jijini Arusha jana. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

## Mamalishe 487 wapewa msaada mitungi ya gesi, majiko

**Na Hamida Kamchalla,** TANGA

WANAWAKE 487 wanaofanya biashara ya mama lishe mkoani Tanga wamenufaika na msaada wa majiko mbadala ya nishati ya gesi, mitungi na meza moja kwa kila jiko.

Mbunge wa Tanga, Ummy Mwalimu, ambaye pia ni Waziri wa Afya, alikabidhi msaada huo jana kwa wanufaika wa msaada huo ulitolewa na Kampuni ya Gesi ya Oryx, wakati wa kongamano la 'Mwanamke Shujaa'.

Kongamano hilo liliwakutanisha wanawake ambao wanafanya biashara zao ndani ya Jiji hilo.

Kabla ya makabidhiano hayo, Waziri Ummy, alisema vifaa hivyo ambavyo vinakwenda kubadilisha maisha ya wanawake hao kiuchumi.

"Kwanza tutaweza kuokoa uchafuzi wa mazingira yetu kwa kutumia nishati safi ambayo ni gesi kupitia wenzetu wa Oryx, lakini pia tutawezesha wanawake kufanya biashara zao katika mazingira mazuri,

"Lakini kubwa tunaamini kuwa wamewapa mtaji wa wanawake kufanya biashara zao na kupata faida zaidi kwa ajili ya kuongeza vipato vyao na familia zao, tunawashukuru sana kampuni za Oryx, Coca Cola pamoja na Idara ya Ustawi wa Jamii ambao walitoa mafunzo kwa wanawake hawa" alisema.

Msimamizi wa Mauzo Kampuni ya Oryx gesi, Kanda ya Mashariki, Shaban Fundi, alisema lengo la kutoa msaada huo ni kuwawezesha wanawake hao kufanya biashara zao kwa kuzingatia nishati safi ya kupikia.

"Hii ni katika kuhamasisha jamii kuacha kutumia kuni na mkaa lakini pia tunajua kwamba kuwawezesha wanawake unawezesha jamii, kwa hiyo Oryx gesi tunaunga mkono juhudi za serikali ambazo inafanya," alisema.

## Wakazi Kijiji cha Msomera wapewa mashamba darasa

**Na Allan Isack,** HANDENI

SERIKALI imetenga mashamba darasa ya ekari 40 katika Kijiji cha Msomera wilayani Handeni mkoani Tanga, kwa ajili ya kuotesha majani ya mifugo yatakayotumiwa na wananchi wa kijiji hicho, pamoja na jamii ya kifugaji ya Wamasai waliohama kwa hiari kutoka eneo la Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA).

Mwenyekiti wa Kijiji cha Msomera, Martin Ole Ikayo, aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari walipotembelea kijiji hicho.

Alisema mashamba darasa hayo yamepandwa majani na serikali ili kuwasaidia wananchi hao hasa wale waliohama Ngorongoro.

Alisema majani hayo yakishakuwa tayari na kufikia hatua ya kuvunwa watayaweka kama akiba kwa ajili ya chakula cha mifugo na yatatumika hasa wakati wa kiangazi kwa kuwa kipindi hicho kuna kuwa na uhaba wa majani ya kulisha mifugo.

Alisema mashamba hayo yako manne, yana ukubwa wa ekeri 10 kwamba majani yamestawi kwa sasa wako kwenye mchakato wa kuvuna na kuhifadhi.

Hata hivyo, alisema mbegu ya majani hayo yanadumu kwa muda wa miaka mitatu.

"Mbegu inadumu ndani ya miaka mitatu ikiota yenyewe kwa hiyo sasa hivi hata wananchi wenyewe wameshaona faida na kila mmoja anatamani kupanda kwenye eneo lake mbegu. Kwa kweli tunaishukuru serikali kwa elimu hii ya mashamba darasa haya kwa kuwa yamekuwa ya mfano na msaada kwa wananchi," alisema.

Aidha, alisema awali kabla ya kuwapo kwa mradi huo wananchi wa eneo hilo hawakuwa na uelewa wa upandaji wa majani ya kulisha mifugo, lakini kwa sasa kila mwananchi anaweza kupanda katika eneo lake. Vilevile alisema awali hawakuwa na elimu ya kwamba majani yanapandwa lakini baada ya elimu hiyo tayari wameshaelimika na mtu binafsi anaweza kuotesha majani.

## Mount Meru wapanua wigo huduma tiba utalii

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

HOSPITALI ya Rufaa ya Mkoa wa Arusha Mount Meru, imeandaa mafunzo ya tiba utalii kwa wadau wa utalii jijini hapa, pamoja na kuongeza uelewa kwa watumishi wa afya wa hospitali hiyo.

Akitoa mafunzo hayo, Mratibu wa Tiba Utalii kutoka Wizara ya Afya, Dk. Asha Mahita alisema kuwa tiba utalii ni kitendo cha kufuata huduma bora ya matibabu katika nchi nyingine.

Alisema Tanzania ikiwa ni kitovu cha utalii Afrika na duniani, tiba utalii inaweza kuwa kichocheo cha kuongeza utalii nchini.

Mganga Mfawidhi wa Mount Meru, Dk. Alex Ernest alisema kuwa Hospitali ya Mount Meru imeongeza wigo wa huduma za bora za afya kwa wageni wanaokuja Arusha kwa ajili ya utalii.

Alisema wameanza kuwapokea wageni wanaotoka nchi mbalimbali wanaofika kupata huduma ya tiba utalii katika Hospitali ya Mount Meru.

Mmoja wa wadau wa utalii aliyepata mafunzo hayo, alishukuru kupata elimu hiyo akisema yamewapa uelewa mzuri ambao awali walikuwa hawana.



# Naibu Waziri akoshwa ushiriki walengwa TASAF katika miradi

**Na Mwandishi Wetu,** MARA

**Wanufaika hao wametekeleza mradi wa barabara katika Mtaa wa Bonde Kati B, Kata ya Kigera, Manispaa ya Musoma mkoani Mara.**

NAIBU Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ridhiwani Kikwete, amewapongeza wanufaika wa Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini (TASAF), kwa kushiriki katika shughuli za maendeleo zenye tija.

Wanufaika hao wametekeleza mradi wa barabara katika Mtaa wa Bonde Kati B, Kata ya Kigera, Manispaa ya Musoma mkoani Mara.

Ridhiwani ambaye yupo mkoani Mara kwa lengo la kutembelea shughuli mbalimbali zinazotekelezwa na TASAF, pia aliwataka walengwa wa mpango huo kuendelea kutumia fursa wanazopewa kujiimarisha kiuchumi ili kuondokana na hali ya duni ya maisha.

"Nawapongeza kwa namna mnavotumia fursa iliyoletwa na Rais Samia Suluhu Hassan kupitia TASAF na kujiondolea hali ya umasikini, serikali inaendelea kuwahudumia wananchi kupitia programu mbalimbali zenye lengo la kuboresha maisha ya wananchi wenye hali duni," alisema.

Aidha, aliwahakikishia walengwa kuwa serikali inafanyia kazi changamoto ya kuchelewa kupata malipo ya ruzuku zao.

Pamoja na mambo mengine, Ridhiwani alikutana na walengwa Joseph Nyawelesa na Zena Abeid kutoka Kata ya Bonde Kati B, ambao wanaendelea na ujenzi wa nyumba za kisasa.

Akizungumza baada ya kukutana na Ridhiwani, Nyawelesa alisema: "Nimeanza ujenzi wa nyumba



naamini ujenzi ukikamilika nitaweza kuondokana na adha yakukosa makazi bora".

Naye Zena alisema ruzuku ya TASAF imemuwezesha kufanya biashara ya uchuuzi wa dagaa ambao umemfanya aweze kuanza ujenzi wa nyumba ya kisasa.

Katika ziara hiyo, Ridhiwani aliahidi kuwaunga mkono walengwa hao kwa kuwanunulia bati ili wakamilishe ujenzi wao ndani ya muda mfupi.



Meneja wa kampuni ya Franone Mining and Gems Ltd, Frank Mziwanda (wanne kushoto), akizungumza na Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Naisinyai, wilayani Simanjiro mkoani Manyara, Agnes Chang'endo (watatu kushoto), baada ya kampuni hiyo kukabidhi msaada wa magunia 120 ya mahindi, magunia 20 ya maharage na ndoo 20 za lita 400 za mafuta ya kula kwa shule mbili za msingi Naisinyai na Oloshonyokie, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# RC aagiza chumba cha kunyonyeshea kijengwe sokoni

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme, ameagiza ujenzi wa masoko yote mapya mkoani humo yazingatie ujenzi wa chumba maalumu kwa ajili ya faragha ya kinamama kunyonyeshea watoto.

Alitoa maelekezo hayo juzi alipofanya ziara ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa ukarabati wa Soko Kuu la Manispaa ya Shinyanga.

Mndeme alisema katika ujenzi wa soko hilo hakuna mahali ambapo ameona kuna chumba maalumu kwa ajili ya kinamama kunyonyeshe Watoto.

"Nimekagua ujenzi wa soko hili sijaona chumba cha kinamama kunyonyeshea watoto wao, hivyo naagiza kijengwe mara moja na hili agizo ni katika masoko yote ambayo yanajegwa hapa Shinyanga," alisema.

Aidha, katika ujenzi wa soko hilo aliagiza kasi iongezwe ili likamilike kwa wakati, na kutoa muda wa mwezi mmoja hadi kufika Oktoba 11 mwaka huu vyumba vya chini viwe vimekamilika kujengwa, vya juu (ghorofa) vikamilike Desemba 11.

"Mimi siwezi kuwapaka mafuta, msema ukweli ni mpenzi wa Mungu, sijaridhishwa na kasi ya ujenzi wa miundombinu ya soko hili mpo nyuma, natoa mwezi mmoja vibanda vya chini



viwe vimekamilika na kuanza biashara,"alisema Mndeme.

Aliwataka wafanyabiashara katika soko hilo wasitumie madalali wala kutoa rushwa, huku akiwasihi kufanya biashara halali.

Ofisa Mipango wa Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga, Michael Makotwe, alisema ujenzi kwa sasa umefika asilimia 57.

Alisema ujenzi huo unahusisha vyumba 106, ambapo vyumba 41 vya chini vipo katika hatua ya mwisho ya ukamilishaji na 65 juu ya ghorofa bado vinaendelea na hatua ya ujenzi.

Alisema ujenzi wa soko hilo utagharimu Sh.bilioni 1.8 kwa kutumia fedha za mapato ya ndani.

Fundi Mkuu wa ujenzi wa soko hilo, Deus Masalu, alisema wameshindwa kukamilisha ujenzi huo kwa wakati kutokana na kukosekana kwa malighafi, zikiwamo kokoto na saruji.

## Polisi wakumbushwa kuzingatia maadili kazini

**Na Remmy Moka,** SAUT

KAMANDA wa Jeshi la Polisi mkoa Mwanza, Wilibroad Mutafungwa, amewataka askari polisi mkoani humo kuzingatia weledi katika utekelezaji wa majukumu yao.

Alitoa kauli hiyo juzi wakati akizungumza na wahitimu ambao ni maofisa ukaguzi wa awamu ya pili 112 katika mafunzo ya utayari ya wakaguzi wa jeshi hilo.

Alieleza kuwa jeshi hilo limejikita katika kuzuia uhalifu pamoja na ulinzi wa mali za raia na kubainisha kuwa hatua za kuzuia uhalifu ndiyo njia pekee ya kuweka amani ndani na nje ya Mkoa wa Mwanza na taifa.

Kadhalika, aliwataka askari hao kuhakikisha wanashirikiana kikamilifu na raia katika kutimiza majukumu yao ikiwamo kudumisha amani.

Vilevile, alivitaka vikundi vya ulinzi shirikishi kuwatumia raia na kuwashirikisha wenyeviti wa serikali za mitaa na watendaji wa mitaa na kata ili kupewa mbinu za namna ya kuweka ulinzi na pia kujadili namna ya uanzishwaji wa vikosi vya ulinzi shiriki.

Aidha, amelitaka Jeshi la Polisi kuwaelimisha wananchi madhara ya kujichukulia sheria mkononi.

Aliwaagiza Maofisa wa Jeshi hilo kuhakikisha hatua za kinidhamu zinachukuliwa kwa wanafunzi ambao hawakushiriki mafunzo hayo ambao idadi yao ni 24 na kuwataka warudie kufanya mitihani.

## Watetezi haki za binadamu wataka migodi itoe ajira vijana

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WADAU wa kutetea haki za binadamu wilayani Kahama mkoani Shinyanga wawashauri wamiliki wa migodi kuhakikisha wanaisaidia serikali katika utoaji ajira kwa vijana, wananchi wanaoishi karibu na maeneo wanapowekeza.

Wamesema kwa kufanya hivyo kutasaidia kupunguza tatizo la vijana wasio na ajira katika maeneo hayo.

Mwanasheria kutoka Shirika la SHIHABI, Alex Makabe, aliyasema hayo alipotembelea mgodi mdogo wa Sheng Long uliopo Kijiji cha Masabi Kata ya Mega Halmashauri ya Msalala.

Katika ziara hiyo aliambatana na wajumbe wa shirika hilo, lengo likiwa kujiridhisha kama mgodi huo unazingatia masuala ya haki za binadamu na sheria za kazi.

Alisema sehemu ambazo zinafanyika shughuli za uchimbaji wa madini vijana wanaozunguka maeneo hayo wanakosa ajira za muda.

Makabe alisema viongozi wa mgodi huo wanapaswa kuhakikisha wanazingatia suala la haki za binadamu kwa wafanyakazi wao ikiwa ni pamoja na mikataba ya ajira, kuunganishwa na mifuko ya hifadhi ya jamii.

# ama

AFYA NA MAZINGIRA

ALHAMISI SEPTEMBA 14, 2023




Ukurasa 14

## Mila na desturi zinavyowaweka hatarini wajawazito wakitelekeza huduma kliniki



## Huduma mpya Afya kwa Wote, ilivyokitanzi kwa haki ya mtoto

Ukurasa 12

KUTAPAKAA UKATILI KONA ZOTE…

# Madhila ya elimu duni, tamaa na umasikini inavyowazamisha vijana

**Na Yasmine Protace**

MFUMO wa maisha sasa unatajwa kuwa kikwazo kwa watoto wa kike na kiume kufanyiwa vitendo vya ukatili wa kijinsia, ambao watoto wa kike wanabakwa, pia wako wanaonajisiwa.

Mwenyekiti wa Kituo Cha Taarifa na Maarifa, Mabibo Dar es Salaam, Rehema Mwinyi, anataja ukatili wa kijinsia unatokana na sababu mbalimbali, ikiwamo mfumo wa maisha ya kila siku.

Anasema, kutokana na kituo chao kuwasaidia wanaofanyiwa ukatili wapate haki, kuna uchunguzi unaofanyika kwa baadhi ya wanaofanyiwa ukatili na kubaini mfumo wa maisha nao unachangia ukatili kufanyika ikiwamo, ndoa.

"Mfumo wa maisha,unakuta watoto wengi,wanakosa malezi,wanakosa chakula na hivyo,wanaamua kutafuta chakula kwa njia ambazo sio halali na hivyo kubakwa au kulawitiwa, ili waweze kupatiwa pesa," anasema.

Katika hilo, wanandoa wanapoachana husababisha watoto kujilea, nayo inachangia watoto kufanyiwa ukatili wa kijinsia.

Pia, uchunguzi umegundua sababu nyingine ni mimba za utotoni, mtoto anayezaliwa analelewa na mtu baki, wakiwamo wazee vijijini, hatua ambayo mtoto huyo anakuwa wa kujiamulia mambo yake, hata anafikia hatua kutojua mipaka kati ya yanayofaa na yasiyofaa kimaisha.

Anashauri elimu iendelee kutolewa, ili kuwanusuru watoto wasifanyiwe matukio ya ukatili, huku kukitajwa ukatili mwingine unaofanywa hasa kwa watoto wa



Watoto wakiwa katika mijumuiko yao. Ustawi wao kimaisha, kwa kiasi kikubwa unategemea mifumo bora ya wazazi na walezi wanaowasimamia. **PICHA: MAKTABA.**

kiume, kutokana na kukosa pesa za kuingia katika mabanda ya sinema, ikiwamo Sh. 200, ambayo ni mvuto mkubwa kwao.

Rehema anasema, sasa nguvu kubwa zinaelekezwa shuleni kwa kuwapatia elimu ya ya jinsia watoto na namna ya kujilinda, ili wasifanyiwe mabaya hayo.

Mtazamo wake ni kwamba, mfumo wa maisha unapobadilika, matukio ya ukatili nayo yanaweze ama kuisha au kupungua.

Anasema, katika ofisi zao huwa wanawapokea watu mbalimbali wenye malalamiko ya ukatili na kuchunguza ukweli, pia sababu za kufanyiwa ukatili huo.

Kaimu Mkurugenzi wa Shirika la Usawa wa Kijinsia Tanzania (SUKITA), Msafiri Mwajuma Mariam, ambaye pia ni Mkuu wa Dawati la Mafunzo na Uelimishaji SUKITA, anasema wanawapatia watoto elimu, jinsi ya kupambana na matukio ya kikatili.

Anaeleza shirika lao lililoanzishwa mwaka 2014, limeshabaini anachokifafanua kuwa ni: "Serikali iliweka nguvu kubwa kwa ajili ya kuwalinda watoto wa kike katika ukatili na wakawasahau watoto wa kiume."

Pia, Mariam anafafanua kutokana na nguvu kubwa kutumika kuwalinda mabinti, sasa adha hiyo inawaangukia watoto wa kiume zaidi, ambao wana kawaida ya kukaa kimya.

"Watoto wa kiume wanaofanyiwa ulawiti hawasemi, kwa kuwa wanaowalawiti wanawaambia wakisema watauawa," anasema.

" Watoto wa kiume wakikosa shilingi 200 kwa ajili ya kucheza 'gemu' au kuingia katika mabanda ya video, hulazimika kufanya mapenzi ili waweze kupata pesa hiyo," anasema.

Kutokana na madhila hayo ya ukatili, anasema taasisi yao imekuwa ikitoa elimu ya watoto jinsi ya kulinda na masuala ya ukatili kijinsia.

" Wanatoa elimu ili iwasaidie wanafunzi wawe mabalozi shuleni na sasa wana mpango wa kwenda sokoni, misikitini na makanisani kwa ajili ya kutoa elimu ya masuala ya ukatili," anasema.

Anaongeza kuwa changamoto anayoiona, ni baadhi ya watu kufanyiwa ukatili kijinsia na kushindwa kutoa taarifa au wengine kumalizia majumbani, ili kesi zisiendelee.

Mariam anasema, matukio ya ukatili wa kijinsia yanatokea baada ya wazazi kutengana na kusababisha watoto kujilea wenyewe.

" Chanzo cha wanawake kutelekeza watoto na kusababisha kukaa na mama wa kambo, nayo inachangia kufanyika ukatili kwa jamii," anasema, akitaja kuwapo kesi za wanawake kudai talaka ili wagawane mali

Anasema ni kitu kinachochangia kutokea tatizo la ukatili, pale watoto wanapoachwa bila ya malezi sahihi.

Katika mchango wao SUKITA, Mariam anasema wameweza kutoa elimu ya afya ya akili, kwa kuwa pia inabainika kuwa sehemu ya matukio hayo ya mauaji na wabakaji.

**MZIZI WA TATIZO**

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Macho kwa Jamii, pia Mwenyekiti wa Kituo cha Taarifa na Maarifa Manzese, Dar es Salaam, Theresia Lihanjala, anasema kukosekana kwa utii kwa Mungu na umasikini, kuna nafasi kubwa ya kutokea ukatili wa kijinsia.

Anasimulia kuwapo vijana wanaopata watoto bila ya kuwa na matarajio, hali inayowafanya kukosa mahitaji muhimu na kuamua kujiingiza katika uhusiano wa kimapenzi.

"Unakuta mtoto kazaa mtoto, kumtunza hawezi anamuachia mtoto wake mtu amlelee na mtoto anapokosa huduma za kimsingi anajiingiza katika uhusiano na hata kufanyiwa ukatili," anasema.

Anaongeza kuwa watoto wengi kutokuwa na malezi, hali inayowachangia kujiingzia bila ya kujua katika makundi yasiyofaa, hata kusababisha wakafanyiwa ukatili mbalimbali.

Hapo Theresia anatumia mfano ulioko Manzese Dar es Salaam anakofanyia kazi, 'mabinti mama' ni wengi; mtoto anakuwa na mtoto.

Katika hilo, anahitimisha kwa ushauri: "Elimu itolewe kwa mabinti mama... elimu hiyo ikitolewa,

Inaendelea Uk. 13

Na Christina Mwakangale

AFYA

# Huduma mpya Afya kwa Wote, ilivyo kitanzi kwa haki ya mtoto

MALENGO ya Maendeleo Endelevu 2030 (SDGs), hususani lengo la tatu ni kuhakikisha uwapo wa Afya Bora na Ustawi. Umoja wa Mataifa (UN), unahimiza uwekezaji kwenye huduma za afya.

Ajenda ya Shirika la Afya Duniani (WHO), mwaka 2018 katika maadhimisho ya Siku ya Afya Duniani, yalilenga kuhamasisha Huduma ya Afya kwa Wote (UHC), pasipo vikwazo vya kiuchumi.

Ripoti ya mwaka 2022 ya Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Idadi ya Watu Duniani (UNDP), asilimia 83 ya watu wenye umaskini uliojikita katika maeneo mbalimbali wako nchi za Afrika zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara, theluthi mbili ya watu maskini wanatajwa wako katika nchi za kipato cha kati na asilimia 83 wako vijijini.

**MTIHANI WA HUDUMA**

Ajenda ya dunia ni kuwa na mfuko wa pamoja wa UHC, kwamba ifikapo mwaka 2030, nchi husika iwe imefikia mpango huo kwa kiwango kikubwa. Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), ndiye mratibu wa azma hiyo nchini.

Ili kufikia malengo hayo, kulitokea mabadiliko ya vifurushi kwa aina ya huduma za matibabu kwa wanachama tangu mwezi Machi mwaka huu, jambo lililoleta taswira na vikwazo.

Sera ya Afya ya Mwaka 2007, inabainisha kwamba huduma za afya kwa wazee, wajawazito na watoto wenye umri chini ya miaka mitano, huduma za matibabu ni bure.

Wanachama walioondolewa kwenye huduma hiyo kutokana na masharti mapya, ni watoto walio chini ya umri wa miaka 18, kundi maalumu linalotambuliwa na Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009.

Kwa sasa, usajili wa watoto wahitaji wa huduma hiyo tangu Machi mwaka huu, wanatakiwa wafikie orodha 100 shuleni, ndipo wajiunge na 'Toto Afya' jambo ambalo walezi, walimu na wazazi wanakwama kulitekeleza.

Takwimu zinaonyesha watoto wengi wanaozaliwa nje ya mfumo rasmi, kama idadi iliyopo ya wanafunzi 9,011 wa shule za msingi na sekondari nchini waliopata ujauzito katika kipindi kati mwaka 2021 hadi 2022 nchini. Wengi wako chini ya umri miaka 18, wameshajifungua na kuishia kwenye kundi la mama walezi pekee na tegemezi kwa familia.

**KUANZA MFUMO MPYA**

Ikiwa imepita miezi mitano tangu kusitishwa kwa huduma ya 'Toto Afya' kwa mtoto mmoja mmoja. Sharti lililopo NHIF, mzazi au mlezi ambaye awali alimlipia mtoto wake kila mwaka Sh. 50,400 'Toto Afya Kadi' kwa ajili ya matibabu yake, sasa hawezi kufanya hivyo.

Anamsajili mwanawe kupitia vifurushi tofauti kwenye kundi la 'Najali Afya' akiwekeza kifurushi cha mtu mmoja na hakimhusishi mtoto au tegemezi thamani yake ni kuanzia Sh. 192,000 hadi Sh. 984,000 kwa mwaka, kulingana na umri wa mhusika. Mdhibiti Mkuu na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali (CAG), anakosoa bajeti ya NHIF, kwamba inakusanya fedha, ila matumizi yao hayana msingi huku wakikopeshana Sh. bilioni 41. Hii ni ripoti yake ya 2022/2023.

Waziri Ummy Mwalimu, anasema, mfuko huo sasa unaelemewa kutokana na kulipa gharama kubwa za Magonjwa Yasiyoambukiza (NCDs), kama kisukari, kiharusi na shinikizo la juu la damu.

Anasema magonjwa hayo yameugharimu mfuko takribani Sh. bilioni 99.09 kwa mwaka 2021/2022. NHIF, ikiwahudumia wanachama milioni 4.33 sawa na asilimia nane ya Watanzania wote milioni 60, asilimia sita wakihudumiwa na Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF).

Waziri anasema, kukwama muswada wa bima afya kwa wote, ni kukosekana kwa chanzo cha uhakika cha fedha.

**KUMNYIMA HAKI MTOTO**

Mnamo Machi 13 mwaka huu, NHIF ilitangaza utaratibu wa malipo ya Sh. 50,400 ya huduma ya 'Toto Afya Kadi', imeondolewa kuanzia Machi 13 mwaka huu, kwa ambao bima zao zimekwisha na wanahitaji kujiunga, wajiunge na mfumo mpya.

Inatajwa, watoto walio chini ya umri huo, hususani wanaougua magonjwa yasiyo ya kuambukiza na mengine sugu ikiwamo moyo, himofilia na kifafa, hulazimika kulipa gharama kati ya Sh. 30,000 hadi 130,000 kila kliniki kwa mwezi, kutegemeana na hospitali.

"Mbali na gharama za dawa alipoumwa mwaka huu, alilazwa kwa siku tatu katika hospitali kubwa maarufu iliyopo Gongo la mboto (jina tunalo) Dar es Salaam, nililipa Sh. 286,000 kwa siku hizo, bado dawa," anasema Belina Brown mzazi wa mtoto Frank, mwenye umri mwaka mmoja na nusu.

Leila Marius mkazi wa Kinondoni, Dar es Salaam, anatamka:"Mwanangu aligundulika kuwa ana matatizo kwenye ubongo baada ya kuugua ugonjwa wa kifafa na kuhitajika kuhudhuria kliniki Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), kila mwezi. Sasa bima yake imekwisha Machi mwaka huu, hivyo ninalipia huduma hiyo kwa fedha taslimu.

"Kila mwezi natakiwa niwe na Sh. 150,000 au 200,000 kwa sababu kuna wakati mwingine dawa alizoandikiwa hazipo Muhimbili, nanunua kwenye maduka ya nje bei ni juu zaidi. Ninafanya kazi yenye mshahara wa Sh. 250,000 kwa mwezi," anasema Leila.

Janela Muagi, mkazi wa Mabibo jijini Dar es Salaam, anasema mtoto wake anaugua ugonjwa wa moyo na kila mwezi anahudhuria kliniki ya watoto wenye ugonjwa huo, hospitali ya Dar Group ambayo ni tawi la Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) na kila mwezi ni Sh. 130,000.

Regina Valence, Mwenyekiti wa Wanawake wa Chama cha Himofilia Tanzania na mzazi wa watoto wawili wanaougua ugonjwa wa himofilia, anasema umoja huo wenye wanachama wanaokadiriwa kufikia 200, watoto walio wengi hawana huduma ya bima afya. "Watoto wetu wao wana kliniki muda wowote akivuja tu damu."

Mkurugezi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga, anasema ni kinyume na Sheria ya Mtoto na marekebisho yake mwaka 2019, Ibara ya 24 ya Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Mtoto ya Mwaka 1989 na Ibara ya 14 ya Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto.

**NINI KIFANYIKE?**

Kamati za Usimamizi wa Vituo vya Afya na Bodi ya Afya kwenye wilaya ambazo husimamia vituo vya afya, zahanati, hospitali za wilaya na zilizopo ngazi ya mkoa au taifa, sasa zinatakiwa ziruhusiwe kisimamia huduma hiyo, iwapo kwenye eneo husika mzazi tayari ana kiasi hicho cha fedha, alipie huduma pale walipo.

Vilevile walimu wa shule wana maoni kwamba, utaratibu huo kwao kwanza ni jambo geni na mzigo kwao kwa kuwa hawajawahi kupewa elimu namna ya kuhamasisha jamii ijiunge.

Pia, inataka serikali ichangie gharama.ya huduma za watoto iwapo mzazi analipia Sh. 50,400 kwa mwaka pia serikali ichangie kiasi kama hicho na jumla iwe Sh. 100,800.



Huduma za mama na mtoto zikiendelea kwenye kituo cha afya, ambao ugharamiaji wake, bima ya afya ni muhimu. **PICHA: MTANDAO.**

## MADHILA YA ELIMU DUNI, TAMAA NA UMASIKINI INAVYOWAZAMISHA VIJANA

INATOKA UK. 11

itasaidia wao kuwaelimisha wenzao na wataacha kuzaa bila ya kufuata utaratibu."

**WANAOGUSWA WANENA**

Mkazi Jamal Juma, ana mtazamo kwamba tamaa nazo zimechangia watoto kufanyiwa ukatili kijinsia, huku Zuwena Juma, akinena matukio ya ukatili yapo katika kona zote za jamii.

"Wanaume nao ufanyiwa ukatili. Unakuta mwanamke analazimisha apewe talaka, huku akitaka mgawanyo wa mali uwe sawa, lakini suala la watoto libaki kulelewa na baba yao.

" Huo ni ukatili pia,mama kuondoka katika ndoa, watoto wabaki na baba yao, kufanya hivyo ni ukatili," anasema.

Jamal Rwey, anataja kuenea mtazamo wa jamii kuona mtoto sio wao wote, bali ni wa mzazi pekee, wakati mwingine mmoja pekee.

Vilevile, ananyooshea kidole tamaa ya mali inavyohusiana na falsafa hasi za kufikia utajiri, ikiwamo kamari za 'ku-beti.'

AFYA

## DAKTARI BINGWA:

# Kuendekeza tabia kula udongo, mkaa kunavyowamalizia damu wajawazito

**Na Rahma Suleiman, Unguja**

"MIMBA yangu ya kwanza nilirukwa na damu; kiasi cha kukaribia kupoteza maisha. Nilipokimbizwa hospitali, daktari aligundua haraka tatizo langu," anasimulia Fatma (jina la pili tunalo) (35), mama wa watoto watatu, mkazi wa Magomeni, mjini Unguja.

"Nilikuwa nakula mchele na udongo na kwamwe, sikupenda kuukosa. Daktari alinishauri niache kutumia mara moja kwa usalama wangu," anaeleza, wakati akizungumza na mwandishi wa makala hii.

Zao la kutii dokezo hilo la daktari, ni kwamba kila kitu kwa ujumla kilibadilika kiafya baada ya mwezi mmoja, kiwango chake cha damu kiliongezeka na afya yake ikaimarika.

Alichopitia Fatma, ndicho wanapitia wanawake wengi wakati wa kipindi cha ujauzito kwa kula vitu visivyo na faida katika kuimarisha afya zao.

Mashavu Kombo, mkazi wa kijiji cha Chaani Mkoa wa Kaskazini Unguja, naye anakabiliwa na tatizo kama la Fatma, kutokana na tabia yake kula mkaa katika ujauzito wake, akinena bila kula mkaa hajisikii kula chochote, kwa sababu anatapika kila mara na kukosa hamu ya kula.

**WATALAMU WA AFYA**

Mtaalamu bingwa wa Afya ya Wanawake na Uzazi, kutoka Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja, Dk. Ummulkulthum Omar, anasema asilimia 14 ya wajawazito wanaofika hospitalini, huwa na kiwango cha chini cha damu.

"Wengi wanaofika hospitali wanakuwa na damu chini ya saba, kiwango ambacho ni hatari kwa afya zao na watoto," anasema, ili mjamzito aweze kujifungua vyema, anatakiwa kuwa na kiwango cha damu zaidi ya 14.

"Kama mjamzito atakuwa na kiwango kikubwa cha damu, kitamsaidia kuokoa maisha yake na mtoto, kwa sababu kipindi cha kujifungua mama hupoteza damu nyingi, hivyo akiwa na damu hafifu anaweza kufariki," anasema Dk. Ummulkulthum.




Mtaalamu wa maradhi ya wanawake na uzazi kutoka Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja, Zanzibar, Dk. Ummulkulthum Omar, akitoa elimu ya afya ya uzazi kwa waandishi wa habari ambao hawapo pichani. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

Mtaalamu huyo anashauri utumiaji wa vitu vinavyotakwa na wajazito hao, udongo na mkaa, kunasababisha upungufu wa damu, pia ni chanzo cha magonjwa yasioambukiza kama shinikizo la damu, ambayo ni hatari kwa maisha ya mjamzito.

"Unapopata shinikizo la damu kuna uwezekano mkubwa kwa mjamzito kupata kifafa cha mimba, ambayo matokeo yake ni kifo. Ni ugonjwa ambao sisi wataalamu tunauogopa kwa sababu nafasi ya mjamzito kupona ni ndogo," anasema.

Aidha, anasema kila wajawazito 10 wanaofariki kutokana na uzazi, wajawazito watatu huwa na tatizo la upungufu wa damu, hivyo anashauri ili kukabiliana na changamoto za uzazi, mjamzito anatakiwa kula vyakula vyenye lishe na hapaswi kukaa na njaa.

"Tunawahimiza wajawazito kula kwa wingi vyakula vya jamii ya mboga, matunda, wanga, soya na nyama, kwa sababau vinasaidia kurutubisha mwili na kuongeza damu," anasema.

Anafafanua, umuhimu wa mjamzito kunywa maziwa kunamuweka mbali na uwezekano wa kutopata kifafa cha mimba, kwa sababu maziwa yana madini ya 'calcium'.

Hata hivyo, ana hoja ya upande wa pili wa shilingi, upatikanaji wa vyakula hivyo unaweza kuwa changamoto kwa wajawazito wengi, kutokana na ukosefu wa kipato.

Hapo ana rai kwa wanaume kutimiza wajibu wao, kwa kuhakikisha mjamzito anapata huduma zote muhimu, ili kuimarisha afya yake na mtoto aliye tumboni.

"Mtoto anayezaliwa na mama, aliyepata matunzo mazuri wakati wa ujauzito, ni tofauti na mtoto aliyezaliwa na mama ambaye hakupata lishe kamili. Uwezo wake wa kufahamu huwa mkubwa zaidi kuliko mtoto aliyekosa lishe akiwa tumboni," anasema.

Dk. Rahila Salim Omar, kutoka Hospitali ya Wilaya Chake Chake, anasema mjamzito anatakiwa kula vyakula vyenye lishe kuanzia siku ya kwanza ya kutungwa mimba hadi kuzaliwa.

"Mama mjamzito anayekosa lishe bora, ana nafasi kubwa ya kuzaa mtoto aliyedumaa na mwenye utapiamlo ambao ni hatari kwa afya ya mtoto," anasema.

Daktari huyo anasema, baadhi ya vyakula vinapunguza madini chuma kwa mjamzito na ni hatari kwao; hapo anaorodhesha udongo, mkaa, soda, kahawa, pombe. Pia, ulaji wa vyakula hivyo unahatarisha watoto kuzaliwa wakiwa na ulemavu wa akili.

**MIKAKATI YA SERIKALI**

Waziri wa Afya, Nassor Ahmed Mazrui, anasema serikali imeongeza bajeti ya afya, ili kukabiliana na changamoto za afya, ikiwamo kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi.

"Bajeti ya wizara imeongezeka kutoka shilingi bilioni 154,027,109,000 mwaka 2022/2023 hadi shilingi bilioni 189,379,436,000 mwaka huu wa fedha na moja ya vipaumbele vyetu ni kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi," anasema.

**WANAHABARI WANAKOSIMAMIA**

Mkurugenzi wa Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (TAMWA-Zanzibar), Dk. Mzuri Issa, anasema baada ya kubaini walakini, anakiri serikali pekee haiwezi kupunguza changamoto zikazowakabili wajawazito, wameanza kuchukua hatua kutoa elimu kwa kwa usahihi masuala ya afya ya uzazi.

"Tumegundua kwamba kuna pengo kubwa la kupata taarifa sahihi za afya ya uzazi kwa wanawake, ambao wakati mwingine huchangia vifo vinavyotokea.

"Hivyo, tunawajengea uwezo wanahabari ili waripoti kwa weledi masuala hayo. Hii itaongeza hamasa kwa wajawazito kuwa na taarifa sahihi juu ya afya zao na kuzitumia," anatamka Dk. Mzuri.

**WASHIRIKA MAENDELEO**

Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Idadi ya Watu la Umoja wa Mataifa (UNFPA) nchini Tanzania, Mark Bryan, anasema shirika hilo litaendelea kuiunga mkono Zanzibar kuzuia vifo vya uzazi.

"Tunachukua kila hatua kupunguza vifo vya mama na watoto kwa vile muonavyo vyanzo vyake vinaweza kuzuilika. Vifo vya uzazi Zanzibar bado ninatoa ishara ya hatari na masuala ya afya ya uzazi, yanaendelea kuwa miongoni mwa sababu zinazoongoza kwa vifo," anatamka Bryan.

**UKUBWA WA TATIZO**

Ripoti ya Wizara ya Afya Zanzibar, katika kipindi cha miaka mitano kuanzia 2017 hadi 2021, kuna vifo 766 vitokanavyo na uzazi vilisajiliwa.

Hata hivyo, vimepungua kwa wastani wa asilimia 30 kutoka vifo 191 mwaka 2017 hadi vifo 134 mwaka 2021.

Ripoti inaonyesha wajawazito wanaopoteza maisha katika vituo vya kujifungulia, imepungua kutoka 70 mwaka 2021 hadi 53 mwaka jana.

Ni kiwango ambacho kikilinganishwa na nchi za visiwa kama Mauritius, Zanzibar iko katika sura ya ubora zaidi.

Kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO), wastani wa wajawazito 800 walifariki dunia kila baada ya dakika mbili mwaka 2020, kutokana na vyanzo vinavyoepukika.

Hata hivyo, ikilinganishwa na nchi kama Comoro; Zanzibar imetajwa kupiga hatua katika kupunguza vifo vya uzazi.

Lengo la tatu la Maendeleo Endelevu ya Dunia (SDGs) ni kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi chini ya 70 kwa kila vizazi hai 100,000 ifikapo 2030.

**NINI KIFANYIKE?**

Dk. Umulkulthum, anasema ili kupunguza tatizo la upungufu wa damu kwa wajawazito na hatimaye vifo, kuna haja kwa serikali kuongeza uwekezaji katika sekta ya afya hasa eneo la uzazi.

Aidha, akashauri serikali za wilaya kuongeza elimu ya afya ya uzazi na lishe bora kutoka ngazi ya elimu ya msingi, kuwajengea msingi imara watoto.

AFYA

# Mila na desturi zinavyowaweka hatarini wajawazito wakitelekeza huduma kliniki

## •Asiyeolewa anahama nyumbani, hospitalini haonekani




Jengo la Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Manyara. **PICHA: JALIWASON JASSON**

**Na Jaliwason Jasson, MANYARA**

MAISHA ya majamzito dhidi ya mila na utamaduni ni tatizo kitaifa, huku mkoani hapa kukiwapo simulizi zenye uthibitisho wake.

Kuna dhana katika jamii za Kiafrika pale mwanamke anapobeba ujauzito kuna jamii inaonekana kama neema kwao, lakini kwa nyinginezo, ujauzito ukibebwa nje ya ndoa, huku ikionekana ni kosa kubwa la kimila, hata kuoanishwa na laana

Ni aina ya uhalisia unaotolewa kutoka kwa mkazi wa kjiji cha Dareda, wilaya ya Babati, Mama Karen Malle, anayesimulia namna mtu anapoolewa, inakuwa rahisi kuhudhuria kliniki, akipewa ruhusa na mume wake kwenda ama zahanati au kwenye kituo cha afya.

Anasema, inapotokea mama asiye na ndoa anabeba ujauzito bila ya kuolewa, wengine hugopa kuhudhuria kliniki, kwa hoja amepata mimba nje ya ndoa na kuna wakati kwa jamii ya makabila yenye asili ya ufugaji, binti mjamzito hufukuzwa kwao.

Mkazi wa Mtaa wa Negamsi, Anna Paul, anasema kuhudhuria kliniki kwake ni jambo jema, kwa kuwa inamsaidia mjamzito kujua hali ya mtoto na kueleza vitu vinavyomsumbua, ili apate ushauri wa kitaalamu.

Samweli Akonay, mkazi wa Nangwa wilayani Hanan'g, ansema wajawazito kuhudhuria kliniki ni muhimu kwa kuwa kliniki ndiko kuna madaktari na wauguzi wenye vifaa vya kisasa vya kumuona mtoto tumboni na kuangalia namna alivyokaa.

Akonay anashauri wanaokwepa kliniki wakiwa wajawazito wanakosea, wanatakiwa kubadilika kukiweka salama kiumbe kilicho tumboni kwao, hali kadhalika usalama binafsi.

Mkazi wa Mtaa wa Hangon A, Goodluck Sendula, anasema kuhudhuria kliniki kunasaidia kujua afya ya mtoto na mama anapewa ushauri wa kitaalamu, ikiwamo yahusuyo vyakula, ili mtoto aweze kukua vizuri.

Hapo anarejea simulizi ya mfano wa jirani yake, aliyeanza kutokwa na damu wakati wa ujauzito, lakini alipoenda kliniki alipewa vidonge akatumia na vilimsaidia, ujauzito ukaendelea na hatimaye akajifungua salama.

**KIOO CHA WATAALAMU**

Mratibu wa Afya ya Uzazi na Mtoto wa Mkoa wa Manyara, Emma Ngatoluwa, anafafanua mjamzito anatakiwa kuanza kuhudhuria kliniki tangu ujauzito ukiwa na miezi mitatu au chini ya miezi hiyo, ikijumuisha wastani wa mara nane mpaka anajifungua, ili aweze kupata huduma zote stahiki.

"Mjamzito anapochelewa kuja kliniki, hatuna cha kumfanya tutampokea na kumhudumia vizuri, ila kuna huduma atakuwa ameishazikosa," anaeleza Ngatoluwa.

Aidha, anasema mjamzito anapowahi anapatiwa dawa za kuongeza damu, madini chuma na huku akishauriwa lishe bora za kutumia.

Mtaalamu huyo anatahadharisha, mjamzito kuchelewa na akawa na vimelea vya maradhi kama malaria na kaswende, inahatarisha kondo la mama na kumuathiri mtoto, akieleza, mahudhurio hayo ndiyo yanawasaidia wajawazito kujua maendeleo yao na watoto walivyokaa tumboni,

Pia, anasema yanawasaidia kujua mahali wanapotakiwa kwenda kujifungua wakati ukifika, anafafanua akisema ujauzito wa kwanza anapofika wakati kujifungua, huelekezwa kwenda kwenye kituo cha afya au hospitali, hawaruhisiwi kwenye zahanati.

Ili kuhakikisha huduma ya kliniki za wajawazito inapewa kipaumbele, anasema kwenye wilaya ya Kiteto zipo baadhi ya kata wanazotoza faini Sh. 50,000 kwa mjamzito asiyehudhuria kliniki au haendi kujifungua kwenye kituo cha afya au hospitali.

Ngatoluwa anasema: "Huduma anayopata mjamzito katika vituo vya serikali anatakiwa aipate vivyo hivyo kwenye vituo vya Afya na Hospitali za binafsi."

**DAKTARI BINGWA**

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Manyara, Dk. Catherine Magali, ambaye ni bingwa wa magonjwa ya wanawake, anasema wajawazito kuhudhuria kliniki ni muhimu kubaini shida za mama na mtoto.

Anasema, mjamzito anapowahi kliniki inamsaidia apimwe wingi wa damu, kujua kama ana kifafa cha mimba, kwa kuwa kinampata mjamzito yeyote, hivyo wanakifanyia kazi mapema.

Dk. Magali anataja kitu kingine, wanamwangalia mgonjwa kama ana malaria, ili waitibu isimharibu mtoto na kumuangalia mtoto alivyokaa, kama amekaa vibaya wanaona namna ya kushughulikia.

Tahadhari ya bingwa huyo, ni kwamba mjamzito anapokuwa na ugonjwa kama kaswende, unaweza kuambukiza na mtoto akaupata kutoka kwa mama au akafa, inaweza kuingia kwenye mishipa ya fahamu ya mtoto na akazaliwa na degedege.

**PENYE TAASISI DINI**

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Misheni ya Dareda, Manyara, inayomilikiwa na Kanisa Katoliki Dk.Joseph Lorri, anasema huduma za kliniki za wajawazito ni bure wanatekeleza sera ya Wizara ya Afya.

Dk. Lorri anasema, wajawazito huwa wanawapatia vipimo vya awali kama vile mkojo, damu, uzito na shindikizo la damu.

Kuhusu wasioenda kliniki na wenza, anasema wanawahudumia, ila wanawahimiza kuambatana na wenza, kwani wananufaika kwa kupewa kipaumbele, kwa sababu nyumbani wanakuwa hawajamuacha mtu.

Mtaalamu huyo naye anatetea hakuna lugha chafu, bali upendo na ushauri wa kuanza kliniki mapema, maana matatizo ya ujauzito yanatofautiana kati ya mtu mmoja na mwingine.

Mkunga wa Zahanati ya Margakan, Philimina Sanka, anatoa takwimu, kuanzia Januari na Agosti mwaka huu, wameshawahudumia wajawazito 380, katika mgawanyo; Januari, Februari na Machi, wako 35 kila mwezi; Aprili ni 40; Mei, 59, Juni, 47, Julai 58 na Agost wako 61.

Sanka anasema vipimo vya maabara na damu, wajawazito wanachangia.

**USHUHUDA WA WAJAWAZITO**

Mkazi wa Sinai, Hawa Juma, anasema alianza kliniki ya ujauzito akiwa na miezi minne, baada ya kulazwa hospitali ya wilaya, ukiwa ni ujauzito wake wa kwanza.

Anasema, huduma anayopatiwa katika zahanati tajwa ni nzuri, huku mkazi wa Hangon, Flora Modi, anasema ameanza kuhudhuria kliniki ya ujauzito ukiwa na miezi nane na alichelewa, kwa kuwa huduma hiyo, baadhi ya hospitali na vituo vya afya vya serikali, navyo vinahitaji malipo.

Utafiti wa Tathmini ya Utoaji Huduma za Afya Tanzania (TSPA) wa mwaka 2014/15 kutoka ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) Ufuatiliaji wa Wajawazito, waliofika kliniki mara ya kwanza walikuwa 1,853.

Utafiti huo ulitoa matokeo ya ushauri wa wajawazito, ambao karibu wateja wote wa kliniki ya wajawazito walipatiwa huduma kwa vitendo.

Inafafanuliwa kwenye utafiti huo kwamba, asilimia 80 kati yao walifanyiwa vipimo vya shinikizo la damu; asilimia 88 walipimwa uzito; na asilimia 96 walipimwa kimo cha mimba; huku asilimia 75 walipatiwa huduma ya vidonge vya madini ya foliki asidi.



# Jafo apongeza Samia kuteuliwa, ataja miradi iliyompa heshima

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Dk. Selemani Jafo, amempongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuteuliwa kuwa Mjumbe wa Bodi ya Ushauri ya Kituo cha Dunia cha Uhimilivu wa Mabadiliko ya Tabianchi (GCA), na kutaja miradi mikubwa mitatu iliyompa heshima hiyo.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa alipokuwa akitoa tamko la Waziri kuhusu Siku ya Kimataifa ya Hifadhi ya Tabaka la Ozoni, Dk. Jafo alisema katika mikutano mbalimbali ya mazingira ya kidunia Rais Samia amekuwa kiongozi wa mfano katika usimamizi wa masuala ya mabadiliko ya tabianchi duniani.

**Kuepuka kutupa ovyo majokofu ya zamani ama vifaa vya kuzima moto vyenye kemikali zinazomong'onyoa tabaka la ozoni au kusababisha ongezeko la joto duniani.**

Alisema Tanzania ni miongoni mwa nchi zinazoigwa mfano katika utekelezaji wa miradi inayopambana na mabadiliko ya tabianchi.

"Utekelezaji wake umeanishwa katika nchi yake ilivyojipambanua katika kupambana na mabadiliko ya tabianchi katika miradi mbalimbali, kwa mfano hivi sasa Tanzania inaigwa mfano kwenye mradi wa ujenzi wa reli ya SGR itakayotumia umeme, kazi ya mradi huu ni kupambana na mabadiliko ya tabianchi," alisema.

Alisema utekelezaji wa mradi wa mabasi yaendayo kasi jijini Dar es Salaam umebeba sifa duniani.

"Uwekezaji mkubwa wa zaidi ya Dola za Marekani bilioni tatu sawa na Sh.Trilioni 6.5 ambazo zinawekezwa kwenye mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere la kuzalisha umeme, hii ni miongoni mwa miradi kimataifa ya kupambana na mabadiliko ya tabianchi,"alisema.

Kadhalika, alisema ndani ya miaka miwili Rais Samia amefanya mapinduzi makubwa ya kibajeti kwenye Wizara ya Kilimo kutoka Sh.Bilioni 294 hadi Sh.Bilioni 970 ambapo fedha hizo zimeelekezwa kwenye miradi ambayo inahimili mabadiliko ya tabianchi.

"Ofisi ya Makamu wa Rais inapenda kumpongeza Rais Samia kwa uteuzi huo na tunapoelekea Siku ya Ozoni Duniani tunasema Tanzania tunajambo la kujivunia katika uongozi mahiri wa Rais Samia kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi," alisema.

Kuhusu Siku ya Ozoni Duniani , alisema wamejipanga kutoa elimu kwa wadau mbalimbali ili kulinda tabaka la ozoni na kuendelea kuhimiza jamii kupunguza shughuli mbalimbali za kibinadamu ambazo zinasababisha mabadiliko ya tabianchi.

Alitoa rai kwa wananchi kuepuka kuingiza nchini gesi zilizopigwa marufuku na vifaa vinavyotumia gesi haribifu kama vile majokofu na viyoyozi yaliyotumika.

Jafo alisema: "Kuepuka kutupa ovyo majokofu ya zamani ama vifaa vya kuzima moto vyenye kemikali zinazomong'onyoa tabaka la ozoni au kusababisha ongezeko la joto duniani."



Mkuu wa wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri (wa pili kushoto), akisikiliza maelezo kwa Meneja wa dampo linalosimamiwa na Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Chidaya Peter (wa pili kulia), baada ya kulitembelea jana. Kulia ni Mkuu wa kitengo cha usimamizi wa taka ngumu na usafi cha jiji hilo, Dickson Kimaro. **PICHA: PETER MKWAVILA**

## DC: W'biashara, TBS shirikianeni kudhibiti bidhaa zenye sumu

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MKUU wa Wilaya ya Singida, Paskas Mragili, amewataka wafanyabiashara wa vipodozi wilayani humo kushirikiana na Shirika la Viwango Tanzania (TBS), kudhibiti bidhaa zenye viambata vyenye sumu.

Alitoa rai hiyo wakati akifungua kikao kilichowashirikisha maofisa wa TBS na wafanyabiashara, lengo kuu likiwa ni kutoa elimu juu ya uelewa kuhusu vipodozi vyenye viambata sumu Mkoa wa Singida.

Mragili alisema TBS ndiyo limepewa jukumu la kusimamia vipodozi hivyo kupitia mabadiliko ya Sheria ya Fedha ya Mwaka 2019 ambapo limekuja na mkakati wa kuelimisha wananchi juu aina ya vipodozi vyenye viambata sumu vilivyopigwa marufuku nchini.

Alisema kuendelea kuviuza na kuvitumia vipodozi hivyo ni hatari kwani wanaliangamiza taifa jambo ambalo ni hatari na halikubaliki, kwamba baada ya mafunzo hayo hategemei kuona bidhaa hizo zikiendelea kuwapo kwenye soko.

Naye, Meneja wa TBS Kanda ya Kati, Nickonia Mwabuka, alisema matumizi ya vipodozi hivyo vyenye viambata vyenye sumu ni hatari kwa afya ya binadamu na vimekuwa vikiwaathiri watu wengi na kuliongezea taifa gharama kubwa ya kuwatibu waathirika na kupunguza nguvu kazi ya taifa.

Mwenyekiti wa Umoja wa Wauzaji vipodozi Mkoa wa Singida, Pili Hussein, aliomba serikali kuwadhibiti wafanyabiashara wakubwa wa bidhaa hizo ambao wamekuwa wakiwauzia.

Alisema: "Tunashindwa kuelewa kuna vyombo husika vya ukaguzi katika Bandari, viwanja vya ndege na mipakani ambako bidhaa hizi zinapitishwa na wafanyabiashara wakubwa na kusajiliwa ambao wanafahamika lakini wanaacha kuwadhibiti hadi zikifika kwetu ndio wanakuja kuzikamata jambo hili siyo zuri kwani linaturudisha nyuma na kufilisi mitaji yetu".

**TBS ndiyo limepewa jukumu la kusimamia vipodozi hivyo na mkakati wa kuelimisha wananchi juu aina ya vipodozi vyenye viambata sumu.**

# SUWASA kutumia mil.88/- kufikisha maji Kata ya Mtipa

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Singida (SUWASA), kwa kushirikiana na Shirika la Dini la Water Aid Society wameanza mchakato wa kufikisha huduma za maji katika eneo la Manga, Kata ya Mtipa Manispaa ya Singida, mradi ambao utagharimu Sh.milioni 88.

Mkurugenzi Mtendaji wa SUWASA, Sebastian Warioba, aliwaeleza madiwani wa Manispaa ya Singida na wajumbe wa Bodi ya mamlaka hiyo jana walipotembelea miradi inayoendelea kutekelezwa na SUWASA katika manispaa hiyo.

Alisema mradi huo utaanza kwa kuchimba mitaro na kulaza mabomba ya maji kwa urefu wa mita 5800 kuanzia eneo la Manguanjuki hadi Manga ambapo utakapokamilika utaongeza kiwango cha upatikanaji wa maji eneo hilo na utachukua siku 90 hadi kumalizika.

Warioba alisema hivi sasa katika Manispaa ya Singida kuna mahitaji makubwa ya maji kutokana na ongezeko la idadi ya watu ambapo kiwango kinachozalishwa kwa siku ni lita milioni 11 wakati mahitaji halisi ni milioni 18 na hivyo kuwa na upungufu wa maji lita milioni saba.

Alisema tatizo la umeme kukatika mara kwa mara imekuwa changamoto inayosababisha wananchi kukosa huduma ya maji na kwamba mradi wa miji 28 utakapoanza utasaidia ongezeko la uzalishaji maji na kufikia lita milioni 30 kwa siku na hivyo kumaliza tatizo hilo na kuwa na ziada ya maji.

Awali, Mkurugenzi wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira, Lunango Muwelu, alisema SUWASA imejipanga kumaliza tatizo la maji kwa kupitia miradi inayoendeleza kutekelezwa katika kata hizo.

Naye, Meya wa Manispaa ya Singida, Yaghi Kiaratu, alishauri SUWASA iweke utaratibu wa kukutana na madiwani angalau mara moja kwa mwaka ili kujua kero za huduma ya maji zinazowakabili wananchi katika maeneo yao.

Kiaratu alitaka mamlaka hiyo kuangalia uwezekano wa kufufua baadhi ya vituo vya kuchotea maji ambavyo havitoi maji ili viwasaidie wananchi wakati wakisubiri mradi wa miji 28 kukamilika.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya SUWASA, Kitila Katala, alisema mamlaka imejipanga kuhakikisha kiwango cha upatikanaji wa maji katika Manispaa ya Singida unafikia kiwango cha asilimia 95 pamoja na kudhibiti upotevu wa maji.





# Madereva, viongozi chupuchupu kuzichapa

Na Nebart Msokwa, MBARALI

MADEREVA wa magari ya abiria yanayofanya safari zake kati ya Jiji la Mbeya na wilaya za Rungwe na Kyela, nusura wazichape na viongozi wao kwenye mkutano mkuu wa umoja wao kutokana na kutoelewana kuhusu mapato na matumizi ya fedha zao.

Madereva hao walikuwa wakiwatuhumu viongozi wao kuwa wametafuna fedha ambazo hazijulikani idadi, huku viongozi hao wakikana kutekeleza kitendo hicho huku wakisisitiza kuwa fedha zipo benki hali iliyozua tafrani.

**Viongozi hao walisimamishwa kwa lengo la kupisha uchunguzi ili kubaini kiasi cha fedha ambazo wametafuna kabla ya kuendelea na hatua zingine...**

Baada ya mvutano wa muda mrefu, madereva hao walikubaliana kuwasimamisha viongozi wote wakiongozwa na Mwenyekiti wao, James Kabolesya na kuchagua uongozi wa mpito ambao utasimamia umoja huo kwa muda wa miezi mitatu.

Viongozi hao walisimamishwa kwa lengo la kupisha uchunguzi ili kubaini kiasi cha fedha ambazo wametafuna kabla ya kuendelea na hatua zingine ikiwemo kuwafikisha kwenye vyombo vya sheria.

Akitoa maelezo kabla ya kusimamishwa kwenye uongozi, aliyekuwa Mwenyekiti wa umoja huo, Kabolesya alikiri kuwepo kwa matumizi ya fedha za umoja huo yasiyoridhisha, huku akiahidi kupeleka nyaraka za matumizi ya fedha hizo.

Alisema atakapokuwa anakabidhi nyaraka za umoja huo kwa viongozi wa mpito atahakikisha anakabidhi na nyaraka za matumizi ya fedha zote za umoja huo ambazo zipo benki na ambazo zimetumika.

Vilevile alisema atakabidhi nyaraka za basi la umoja huo ambalo madereva walilalamika kuwa mapato yake hayajulikani na hata nyaraka za umiliki hawajui zilipo.

Aliwaomba madereva hao waendelee kushirikiana naye kwenye majukumu mbalimbali ya kijamii na kwamba hawatakiwi kuchukiana kwa sababu ya madaraka na migongano ya wachache.

Baadhi ya madereva walisema viongozi hao wamekuwa waanyonyaji na wamesababisha upotevu wa fedha nyingi za chama hicho hali ambayo inaweza ikasababisha umoja huo kuvunjika.

Mmoja wa madereva hao, Victor Ezekiel, alisema viongozi hao wamekaa madarakani miaka saba lakini fedha ambazo zipo benki ni Sh. milioni tisa pekee ambazo hata hivyo hawana uhakika kama zipo ama wanadanganya.

Alisema viongozi waliokuwa wamechaguliwa kusimamia kwa muda wa miezi mitatu pekee walikusanya zaidi ya Sh. milioni 81 jambo ambalo liliwatia wasiwasi kwamba fedha zilizotafunwa na viongozi hao ni nyingi zaidi.

Naye Baraka Mwaipungu alisema viongozi wa umoja huo wanatakiwa kushughulikiwa kwa maelezo kuwa wasipofanya hivyo kila kiongozi anayeingia madarakani atakuwa anatafuna fedha bila woga.



Baadhi ya maofisa ushirika wa halmashauri mbalimbali za mkoa wa Mbeya, wakishiriki mafunzo kuhusu mikopo mbalimbali ya kuendeleza kilimo inayotolewa na Benki ya Maendeleo ya Kilimo nchini (TADB), mkoani humo juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Wananchi kicheko serikali ikijenga daraja

Na Nebart Msokwa, MBEYA

WAKAZI kutoka vijiji vya Swaya na Nsenga katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wameondokana na kero ya muda mrefu ya kukosa mawasiliano ya barabara kutokana na kukosekana kwa Daraja la Mto Nsenga, baada ya serikali kukamilisha ujenzi wa daraja hilo.

Wakizungumza baada ya daraja hilo kuzinduliwa na Mwenge wa Uhuru, wananchi hao walisema daraja hilo litasaidia kuinua shughuli zao za kiuchumi na kijamii ikiwemo usafirishaji wa mazao ya kilimo na upatikanaji wa huduma zingine.

Mmoja wa wananchi hao, Joseph Enock, alisema wamekuwa wakipata shida kusafirisha mazao yao kutoka mashambani kwenda kwenye masoko kutokana na kutokuwepo daraja hilo. Alisema baada ya kukamilika kwa daraja hilo sasa watakuwa wanasafirisha mazao hayo kwa gharama nafuu na kwa wakati tofauti na ilivyokuwa awali.

Naye Vumilia Wilson, alisema daraja hilo litawasaidia wanawake kuzifikia huduma za afya kirahisi kwa maelezo kuwa walikuwa wanapata shida ya usafiri kwenda kwenye vituo vya afya.

Meneja wa Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA), Mhandisi Seleman Mziray, alisema daraja hilo ni sehemu ya jitihada za serikali kuwaunganisha wananchi na huduma mbalimbali za kijamii.

## Taasisi zaungana kupambana na ugonjwa wa wanyama

Na Mwandishi Wetu

WAFUGAJI nchini wataanza kupata ahueni ya mifugo yao kutofariki kutokana na ugonjwa wa 'Trypanosomiasis' baada ya taasisi tatu kuungana ili kupambana kuutokomeza.

Ugonjwa huo huathiri wanyama ikiwamo ng'ombe, nyati, kondoo, mbuzi, farasi, nguruwe, mbwa na aina nyingine za wanyama.

Pia, husababisha hasara kubwa za kiuchumi kwa mifugo kutokana na mifugo kupungua damu, kudhoofika sana na kuleta athari kwa uzazi.

Hivyo, ugonjwa huo kwa sasa unaenda kutokomezwa baada ya taasisi ya The Bill and Melinda Gates Foundation, ofisi ya Serikali ya Uingereza inayoshughulika na mambo ya nje, Jumuiya ya Madola na Masuala ya Maendeleo pamoja na kampuni za Boehringer Ingelheim na GALVmed kutangaza kuunda ubia mpya wa kupambana na ugonjwa huo.

Boehringer ni kampuni inayojishughulisha na afya na dawa za binadamu na Wanyama, GALVmed imejikita katika utafiti na uzalishaji wa bidhaa za wanyama zikiwemo dawa na chanjo.

Taarifa iliyotolewa jana na Boehringer Ingelheim imesema taasisi hizo zitafanya utafiti na kushirikiana na miradi mingine ya kitaaluma na ya kimataifa kutafuta ufumbuzi wa kukabiliana na ugonjwa huo hatari.

Maambukizi yasababishwayo na 'Trypanosoma vivax' hutokea pia Kaskazini mwa Amerika ambapo husambazwa na wadudu wanaong'ata kama vile nzi wakubwa na hivi karibuni umeripotiwa huko Mashariki ya Kati.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa vimelea hivyo huingia mishipa ya damu ya mnyama aliyeng'atwa na kuzaliana.

Kadhalika, ugonjwa huo inakadiriwa kuua kiasi cha ng'ombe milioni tatu kila mwaka duniani. Hasara zinazohusishwa moja kwa moja na kupungua kwa uzalishaji wa nyama na maziwa, pamoja na gharama za kutibu na kuthibiti mbung'o na ndorobo zinakadiriwa kufikia Sh. trilioni 2.6 kwa mwaka.

## Wazazi waonywa tabia kushawishi watoto kufeli mitihani

Na Elizabeth John, NJOMBE

WAZAZI na walezi katika Halmashauri ya Mji wa Njombe, wametahadharishwa kuacha tabia ya kuwashawishi watoto kufeli mitihani kwa makusudi kwa matarajio ya kuwapeleka kufanya kazi za ndani kwenye mikoa mingine.

Marufuku hiyo ilipigwa na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji wa Njombe, Erasto Mpete, wakati akizungumza na vyombo vya habari juu ya maandalizi ya halmashauri hiyo kwa watoto wote wanaokwenda kuanza kufanya mitihani ya darasa la saba.

Alisema Mkoa wa Njombe siyo kiwanda cha kuzalisha wafanyakazi wa ndani na hivyo wataanza kuwachukulia hatua za kisheria wazazi ambao wanawashawishi watoto.

"Kuna wazazi wengine wanataka watoto wao wakimaliza tu darasa la saba kama ni wasichana wanataka wawe ni ma-house girl (dada wa kazi) na kama ni wavulana wawe house boy, niwaomba sana wazazi kama elimu ni ufunguo wa maisha ni jukumu la mzazi kuhakikisha mtoto anafanya mtihani na anafaulu," alisema Mpete.

Mpete alisema pia wazazi wanapaswa kuacha kuwagombeza au kuwaadhibu watoto kwa kipindi hiki wanachofanya mitihani ili waweze kuwa vizuri kiakili na kufaulu mitihani yao.

Kwa mujibu wa Ofisa Elimu Msingi wa Halmashauri ya Mji wa Njombe, Fider Kiharamba, alisema wanafunzi 4,871 wanatarajia kufanya mtihani wa mwisho wa kuhitimu elimu ya msingi.



## Serikali yakaa mguu sawa uboreshaji afya ya msingi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Afya Zanzibar imesema kuwa Serikali imeandaa mkakati maalumu wa kuboresha huduma za afya ya msingi ili kutoa huduma bora kwa wananchi.

Hayo yamesemwa katika kikao cha Baraza la Wawakilishi na Waziri wa wizara hiyo, Nassor Ahmed Mazrui wakati akijibu swali aliloulizwa na mwakilishi wa Kimembe Samaki, Haroub Suleiman, aliyetaka kujua hatua zitakazochukuliwa katika kukifanyia ukarabati Kituo cha Afya Kiembe Samaki ambacho kimechakaa.

Mwakilishi huyo alisema kwamba kituo hicho kipo katika hali mbaya sana na hatarishi kwa wauguzi na wagonjwa wanaokwenda kupata huduma.

Alisema: Je? Serikali ina mkakati gani wa kuondosha changamoto katika kituo hicho.

Akijibu swali hilo, Waziri Mazrui alisema miongoni mwa mikakati iliyopo ni kuvifanyia ukarabati mkubwa na baadhi ya vituo kuvijenga upya Unguja na Pemba.

Alisema Kituo cha Afya Kiembe Samaki kipo katika orodha ya vituo vya afya vilivyoingia kwenye mpango huo na fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mkakati huo tayari zimeshapatikana na kazi hiyo itaanza katika mwaka huu wa fedha.

Mazrui alisema Zanzibar vituo vya afya vya serikali vitavyotoa huduma ya afya ngazi ya msingi ni 168 na baadhi ya vituo hivyo vitahitaji kufanyiwa matengenezo kutokana na kuchakaa kwa sababu ya miundombinu yake ni ya muda mrefu.

**Kituo cha Afya Kiembe Samaki kipo katika orodha ya vituo vya afya vilivyoingia kwenye mpango huo na fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mkakati huo tayari zimeshapatikana na kazi hiyo itaanza katika mwaka huu wa fedha.**

# Walia gharama kugombea Uchaguzi Mkuu 2025

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WANAWAKE wenye nia ya kugombea nafasi za uongozi katika uchaguzi mkuu ujao wameiomba serikali kuifanyia marekebisho Sheria ya Uchaguzi Zanzibar, ili waweze kumudu gharama za kugombea nafasi za uongozi zilizowekwa.

Waliyasema hayo wakati wakizungumza katika mkutano wa wadau juu ya kujadili changamoto za ushiriki wa wanawake kwenye masuala ya uongozi na demokrasia uliondaliwa na Jumuiya ya Wanasheria Wanawake Zanzibar (ZAFELA).

Halima Ibrahim kutoka Chama cha ACT-Wazalendo alisema miongoni mwa changamoto zinazowakabili wanawake ni hali ya kiuchumi, hivyo ni vyema sheria ya uchaguzi kufanyiwa marekebisho ili wanawake kumudu gharama.

Alizitaja miongoni mwa gharama hizo ni uchukuaji wa fomu ya kugombea nafasi ya uongozi ikiwemo uwakilishi, udiwani na urais pamoja na gharama za pingamizi.

Kwa mujibu wa Sheria ya Uchaguzi gharama za uchukuaji wa fomu kwa nafasi ya uwakilishi ni Sh.200,000, udiwani Sh.30,000 na Urais Sh. 2000,000 na kwa upande wa gharama za pingamizi ni Sh.30,0000, kwa nafasi ya uwakilsihi ni Sh. 50,000 kwa udiwani.

Halima alisema hali za kiuchumi wa wanawake ni ndogo, hivyo ni vyema gharama hizo kupunguzwa au kuondoshwa ili wanawake wengi waweze kujitokeza kugombea nafasi za uongozi bila ya vikwazo vya kiuchumi.

Akitoa ufafanuzi wa gharama hizo, Ofisa Uchaguzi wa Wilaya ya Magharib A Unguja, Suleiman Hassan Haji alisema tume haipendi watu kuwekeana pingamizi lakini suala hilo ni la vyama vya siasa, hivyo gharama hiyo itasaidia kutowepo kwa dhamana zisizo za msingi.

"Haijawahi kutokea ofisa wa tume kumpinga mgombea bali wagombea kwa wagombea wenyewe ndiyo wanaowekeana pingamizi..licha ya wadau kuona gharama za pingamizi ni kubwa lakini idadi ya wanasiasa wanaoekeana pingamizi ni nyingi" alisema.

Kuhusu gharama za uchukuaji wa fomu alisema gharama zilizowekwa kwa upande wa nafasi ya uwakilishi, ubunge na udiwani alisema fedha hizo ni kama dhamana ili mgombea akifikisha asilimia 10 ya kura alizopata katika uchaguzi mkuu, kwamba hurejeshewa fedha zake na kama hakufikisha fedha hizo huenda katika mfuko wa hazina ya serikali.

Mkurugenzi wa Jinsia kutoka Wizara ya Maendeleo ya Ustawi wa Jamii, Wazee na Watoto, Siti Ali Abasi, alisema wanawake wapewe uhuru wa kufanya kazi ili kuwa na uwezo wa kipato cha fedha na kumudu gharama za kugombea nafasi za uongozi.

"Kama tunataka kuwavuta wanawake huu ndio wakati sahihi wa kuwajengea uwezo, tusisuburi kipindi cha uchaguzi kwa sababu uchaguzi unahitaji maandalizi ya mapema," alisema Siti.

Naye Mkurugenzi wa (ZAFELA), Jamila Mahmoud, alisema licha ya vikwazo vilivyopo dhidi ya wanawake katika masuala ya uongozi lakini wasivunjike moyo katika harakati za kuwania uongozi.

Alisema licha ya jitihada mbalimbali zinazofanyika katika kumuwezesha mwanamke kugombea lakini bado kuna vikwazo ikiwemo vya kimifumo, kisheria, kanuni na sera katika kuleta usawa wa kijinsia.

Mkurugenzi wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA, ZANZIBAR), Dk. Mzuri Issa alisema wanawake wanakabiliwa na changamoto nyingi ambazo zinahitaji kufanyiwa kazi ili kushinda katika kugombea nafasi za uongozi.

Alivitaja vikwazo hivyo ni vya kiuchumi, kimtandao, rushwa na kutokuwepo kwa sera za kijinsia kwa vyama vya siasa.




Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye (kushoto), akifurahia jambo na Mkuu wa Kitengo cha Biashara cha Tigo Business, Kadambara Maita, wakati wa kongamano la siku mbili la 'Connect to Connect' (C2C), lililoandaliwa na wizara hiyo kwa kushirikiana na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano Zanzibar, mjini Unguja hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Katibu Mkuu Kiongozi ataja sifa za APRM katika maendeleo

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU Mkuu Kiongozi, Mhandisi Zena Ahmed Said amesema kuwa Taasisi ya Mpango wa Hiyari wa Nchi za Umoja wa Afrika Kujitathmini katika vigezo vya Utawala Bora Tanzania (APRM) ni chombo muhimu kwa wananchi na serikali kukitumia katika kuimarisha maendeleo.

Alisema ni vyema kuitumia taasisi hiyo kutathmini mambo yaliofanywa na serikali kwa lengo la kuimarisha maeneo ambayo yana changamoto na kuongeza nuru katika maeneo ambayo serikali inafanya vizuri zaidi.

Aliyasema hayo alipokutana na ujumbe kutoka APRM Tanzania ambao walifika Ikulu Zanzibar kwa lengo la kujitambulisha pamoja na kuelezea dhana nzima ya APRM na mikakati ya kuelekea katika ripoti ya pili ya tathmini ya utawala bora Tanzania.

Mhandisi Zena alisema Serikali ya Zanzibar na ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imefanya mambo mengi mazuri na makubwa ambayo yanahitajika kuzungumzwa ili wananchi wa Tanzania na dunia ielewe kwa namna gani Tanzania imepiga hatua katika masuala ya utawala bora.

Aidha, alisema Serikali ya Zanzibar ipo tayari kutoa ushirikiano ambao APRM Tanzania inahitaji katika kuhakikisha kuwa taarifa za Zanzibar zinapatikana kwa wepesi na kwa wakati ili zisaidie katika uandishi wa ripoti hiyo.

Hivyo, aliitaka APRM kuhakikisha wanawafikia wadau muhimu wakiwemo wabunge na wawakilishi ambao wanafanya kazi karibu na wananchi.

Naye, Katibu Mtendaji wa APRM Tanzania, Lamau Mpolo alisema kuwa taasisi hiyo ipo katika maandalizi ya kuandaa na kuandika ripoti ya pili ya tathmini ya utawala bora nchini, hivyo amewaomba wadau, watendaji wa Serikali na wananchi kutoa ushirikiano endapo wataalamu wa kukusanya taarifa watafika katika maeneo yao.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA VYETI



**MUSA SAIDI MDOGO** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.1102-0053** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **MAHUTA SECONDARY SCHOOL** mwaka 2005 , cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S.0338-0580** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **NDANDA HIGH SCHOOL** mwaka 2008 na **CHETI CHA UALIMU** chenye usajili namba: **E0538-0104** kilichotolewa na MTWARA TTC mwaka 2011. Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/KIN/12285/2023**

## KUPOTELEWA KWA VYETI.



**SENI LIMBU TALAMBA** Anatangaza kupotelewa na Bahasha yenye nyaraka mbalimbali kikiwemo Cheti cha kidato cha Nne chenye Index namba **CS110016040** cha Mwaka 2011 Meatu Secondari kilichopotea Mwaka 2020 akiwa Safarini. Kwa yeyote atakaeviona anaobwa kuwasiliana na Seni Limbu Talamba kwa Namba **0742596039**
**SIM/MEA/RB/544420/2020**

## KUPOTELEWA NA CHETI



**JENIFA STEWARD KIHALI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.0275/0010** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **GLENRONS SEKONDARI** mwaka 2021. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/UBU/11570/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MODEST KENETH MWANDEMELE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T798DKZ** aina ya **TOYOTA WISH,** Chassis No. **ZNE100241944.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu.
Taarifa ya polisi:
**PHQ/DOD/DOD/2655/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JOHN SELLA HAYQARU** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **LANDROVER** yenye usjili namba **T 385 ADC** , CHASSIS NAMBA: **JTEBB71J804000819** na ENGINE NAMBA: **1HZ0637131.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**PHQ/ARU/ARU/2173/2023**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya TEMEKE**

**Kituo cha JUMUISHI Mkoa DAR ES SALAAM**

**Usimamizi wa Mirathi Na. 1169/2023**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU MOHAMED SALUM KAPERA**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA SALUM MOHAMED KAPERA**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 16 Mwezi wa 10 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;** Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

**Imetolewa leo tarehe 13 Mwezi wa 09 Mwaka 2023.**

HAKIMU

**IN THE DISTRICT COURT OF KOROGWE**
**AT KOROGWE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 28 OF 2023**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE BROWN CHARLES KALINGA**

**AND**

**IN THE MATTER OF AN APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY BEATRICE BROWN KALINGA**

**GENERAL CITATION**

ALL PERSONS Claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 12th day of OCTOBER, 2023.

Dated at Korogwe this 12th Day of SEPTEMBER, 2023

RESIDENT MAGISTRATE
KOROGWE

**IN THE DISTRICT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 91 OF 2023**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE JOHN DAVID NGANILE**

**BY**

**JACKILINE JOHN DAVID NGANILE..........................................PETITIONER**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules GN 369 of 1963)**

All persons claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 27 day of 09...............2023

Dated at Dodoma this 13 day of 09.........................2023

RESIDENT MAGISTRATE
RESIDENT MAGISTRATE I/c
DODOMA REGION

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 120 OF 2023**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE ELISI MASUDI CHING'OLE**

**AND**

**IN THE MATTER OF AN APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION**

**BY MAGRETH MASUDI CHING'OLE**

**GENERAL CITATION**

ALL PERSONS Claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Admirations made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 2 day of 10, 2023.
Dated at Dodoma this 07th Day of September, 2023

PETITIONER

**WIZARA YA ARDHI,NYUMBA NA MAKAZI**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA YA MASWA. LILILOPO MASWA.**

**MAOMBI MAKUBWA NA.53 YA MWAKA 2022**

**KATI YA**

**KULWA DANGA..............MLETA MAOMBI**

**DHIDI YA**

**JILUGALELA DANGA ....MJIBU MAOMBI**

**WITO/TAARIFA**

**Kwa: JILUGALELA DANGA POPOTE ALIPO KATIKA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA.**

Kwa kuwa mwombaji hapo juu amefungua Maombi dhidi yako katika Baraza hili la wilaya ya Maswa.Maelezo ya madai yanaweza kupatikana hapa Barazani.Unatakiwa kuleta hapa Barazani utetezi wako wa maandishi(WSD)kabla ya tarehe 19.09.2023.

Pia unajulishwa kuwa Maombi haya yamepangwa kutajwa siku ya tarehe 19.09.2023 saa 2;30 asubuhi mbele ya Mhe.J.T.Kaare Mwenyekiti,Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya-Maswa.

Na pia unafahamishwa kuwa iwapo utakadi wito huu na kushindwa kufika siku iliyopangwa,Baraza litalazimika kusikiliza Maombi haya upande mmoja na kutoa uamuzi dhidi yako.

**IMETOLEWA kwa MKONO wangu na MHURI wa Baraza hili leo tarehe 30.06.2022**

J.T.KAARE
MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
MASWA

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**NAFTAL RASHID KIHWELO**
ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA BAJAJI YENYE USAJILI **MC 633CBQ** AINA YA **TVS**
RANGI YA KIJANI.YEYOTE ATAKAEFANIKIWA KUIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KILICHOPO
KARIBU NAE POLISI JALADA NAMBA **PHQ/IRI/IRI/853/2023.**

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 114 OF 2023**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE PETER KALEBI LAZARO**

**AND**

**IN THE MATTER OF AN APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY AYUBU PETER KALEBI**

**GENERAL CITATION**

ALL PERSONS Claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Admirations made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filled on or before the 04 Day of 10, 2023.

Dated at Dodoma this 28 Day of August, 2023

PETITIONER

RESIDENT MAGISTRATE
RESIDENT MAGISTRATE I/c

**THE REGISTRATION OF DOCUMENTS ACT**
**[CAP.117]**
**CHANGE OF NAME BY DEEDPOLL**

**BY THIS DEED, I' LILIAN HASSAN MFYOA of P.O.BOX DAR ES SALAAM, DO HEREBY** wholly, absolutely and utterly renounce, relinquish and abandon the use of my former names of **RUKIA HASSAN HOTTI** and adopt as from the date of this deed poll and in substitution of my former name, the name of **LILIAN HASSAN MFYOA.**
The reasons for the change of my names are that there were some faults occurred during registration of my **PPF number 87587** were my names read **RUKIA HASSAN HOTTI** instead of **LILIAN HASSAN MFYOA** as it shows on my citizen identity card number **19580930-14122-00001-11.**
For the purpose of evidence of such determination, I, hereby **DECLARE** that I shall at all times hereinafter in all records, deed, documents and other writings and all in all action, suits and proceedings as well as in all Public and Private dealings and transactions and creations whatsoever use and subscribe the said name of **LILIAN HASSANMFYOA** as my name in lieu of and in substitution for my former names of **RUKIA HASSAN HOTTI.**
**AND I HEREBY** expressly authorize and require all and every person and whatsoever at all times after the date hereof to designated, describe and address me by the adopted name of **LILIAN HASSAN MFYOA.**
**IN WITNESS WHEREOF, I** have set my hand at Dar es Salaam, and I hereon substitute my old names of **RUKIA HASSAN HOTTI** by new name of **LILIAN HASSAN MFYOA.**

SIGNED and DELIVERED by the said
LILIAN HASSAN MFYOA
who is known to me personally/identified
to me by..............................the latter
being known to me personally in my
presence this......day of..........2023.

DEPONENT



Name:
Signature:
Postal address:
Qualification:

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**NAFTAL RASHID KIHWELO**
ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA BAJAJI YENYE USAJILI **MC 633CBQ** AINA YA **TVS**
RANGI YA KIJANI.YEYOTE ATAKAEFANIKIWA KUIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KILICHOPO
KARIBU NAE POLISI JALADA NAMBA **PHQ/IRI/IRI/853/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**FEDDY ANAELI MWANGA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T762AKM** aina ya Suzuki Pick-up, Chassis No. **SJ40700857.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu.
Taarifa ya polisi:
***PHQ/DOD/DOD/2676/2023***


***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 00745 700 710.***

**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**

**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Rwanda kujenga kinu cha nyuklia kuzalisha umeme

**KIGALI, Rwanda**

SERIKALI ya Rwanda imetia saini ya makubaliano na shirika la 'Dual Fluid Energy' kutoka mataifa ya Canada na Ujerumani, ili kuanzisha ujenzi wa kinu cha nyuklia kitakachotumika kuzalisha umeme na ambacho kitakuwa tayari kwa majaribio mwaka 2026.

Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni hiyo, Goetz Ruprecht, alisema jana, mjini Kigali, kuwa aina mpya ya vinu hivyo, vinaweza kutumiwa kuzalisha umeme, gesi ya haidrojeni na mafuta yaliyosindikwa kwa gharama ndogo kuliko mafuta ya visukuku.

Waziri wa miundombinu wa Rwanda, Ernest Nsabimana, alisema matumizi ya nishati ya nyuklia yatatoa chanzo thabiti na cha kuaminika cha umeme, kupunguza utegemezi wa mafuta na kusaidia kukidhi mahitaji yanayoongezeka ya nishati.

Nsabimana alieleza kuwa kujumuisha nyuklia katika jumla ya vyanzo vya nishati kutasababisha kuwa na aina mbalimbali za vyanzo vya nishati, kuimarisha usalama wa nishati na kupunguza hatari ya uhaba wa usambazaji.

Pia ilielezwa kuwa awali mwaka 2019, Rwanda ilitia saini mkataba wa kuanzisha vinu vya nyuklia kwa ushirikiano na wakala wa nyuklia wa Russia Rosatom, jambo lililozusha upinzani mkali hasa kuhusu hatari zinazohusiana na masuala ya kiusalama.

Rais wa chama kikuu cha upinzani nchini humo cha 'Democratic Green Party of Rwanda', Frank Habineza, aliiambia shirika la habari la AFP kuwa makubaliano kati ya serikali na Kampuni ya 'Dual Fluid Energy' ni hatari na kwamba hayana tofauti kubwa na makubaliano ya mwaka 2019 kati ya serikali ya Kigali na wakala wa nyuklia kutoka Russia.

Habineza alisisitiza kwamba "Hakuna utafiti unaoweza kunishawishi kuwa kuna mahali katika nchi hii ambako kinu cha nyuklia kinaweza kujengwa bila kuyaweka maisha ya watu hatarini."

Bodi ya Nishati ya Atomiki ya Rwanda ikishirikiana na Kampuni hiyo wamebaini kuwa miradi yao ni salama na wala si tishio kwa watu au mazingira.

Katika taarifa yao ya pamoja walieleza kuwa "Kinu chetu cha majaribio ni kifaa kidogo chenye chembechembe ndogo za mionzi. Kwasababu mradi huu si tishio kwa mazingira."

Aidha, taarifa hiyo ilisema hata ikitokea mlipuko kwenye kinu hicho au kwenye jengo lenyewe, basi ni kiwango kidogo mno cha mionzi ndicho kitakachotawanyika.

Afrika Kusini ndio nchi pekee barani Afrika iliyo na mpango wa nyuklia wa kiraia, na vinu vyake viwili vimekuwa vikifanya kazi kwa zaidi ya miaka 30 na kuzalisha megawati 1,860 za umeme, ikiwa ni sawa na karibu asilimia nne ya nishati yote inayozalishwa nchini humo.

**DW**



Mfano wa kinu cha Nyuklia kinachotarajiwa kujengwa nchini Rwanda. **PICHA MTANDAO.**

# Ufaransa yaitaka Niger kumuachia ofisa wake

**PARIS, Ufaransa**

WIZARA ya Mambo ya Nje ya Ufaransa imesema kwamba ofisa wake mmoja amekamatwa na serikali ya kijeshi ya Niger, huku ukiomba utawala wa kijeshi nchini humo kumuachia mara moja.

Utawala huo uliofanya mapinduzi Julai, mwaka huu na kumuondoa madarakani Rais Mohamed Bazoum, aliyechaguliwa kidemokrasia, uliamuru maofisa wa Ufaransa kuondoka nchini Niger, lakini Ufaransa haikutii amri hiyo ikisema kwamba utawala huo sio halali.

Kupitia ujumbe wa X, iliyojulikana kama Twitter, wizara hiyo ilisema kwamba Stephane Jullien, ambaye ni mshauri wa raia wa Ufaransa waliopo nje ya nchi alikamatwa Ijumaa iliyopita, wakati ikiitisha kuachiliwa kwake.

Rais wa Ufaransa Emmanuel Macron, alisema kwamba Balozi wa Ufaransa ataendelea kubaki Niger licha ya kuombwa aondoke na utawala huo wa kijeshi.

Aidha, Ufaransa imekuwa ikisisitiza kwamba inatambua utawala wa Bazoum ambaye ameendelea kushikiliwa na utawala huo, huku taifa hilo likiwekewa vikwazo na mataifa ya Magharibi pamoja na mashirika ya kieneo.

**VOA**

**Utawala huo uliofanya mapinduzi Julai, mwaka huu na kumuondoa madarakani Rais Mohamed Bazoum, aliyechaguliwa kidemokrasia, uliamuru maofisa wa Ufaransa kuondoka nchini Niger, lakini Ufaransa...**

# Korea Kaskazini yamuunga mkono Putin

**MOSCOW, Russia**

KIONGOZI wa Korea Kaskazini Kim Jong-un amesema kwamba anaunga mkono uvamizi wa Russia nchini Ukraine, huku Putin akieleza kuwa taifa lake limeibuka katika mapambano ya kulinda mamlaka yake na usalama dhidi ya vikosi vya kivita.

Hayo yalibainishwa jana baada ya viongozi hao kukutana na kufanya mazungumzo kuhusu mahusiano ya kibiashara na mambo ya kimataifa katika kituo cha kurushia vyombo vya anga.

"Korea Kaskazini inaunga mkono maamuzi yote yaliyochukuliwa na Rais Putin," alisema.

Aidha, wadau mbalimbali wakiwemo Washington, walibainisha kwamba huwenda mazungumzo hayo yakasababisha kufikiwa makubaliano ya uuzaji wa silaha ili kusaidia mashambulizi ya Russia nchini Ukraine. Kwa mujibu wa mashirika ya Russia, Rais Putin, alitangaza kuwa taifa lake litaisaidia Korea Kaskazini kutengeneza satelaiti tena.

Ilielezwa kuwa Rais Kim Jong-un amefanya ziara yake ya kwanza nje ya nchi tangu kuanza kwa janga la UVIKO-19. Na kwamba tayari alikuwa amekutana na Vladimir Putin wakati wa safari yake ya awali nje ya nchi, huko Vladivostok mwaka wa 2019.

Washington inahofia kwamba Urusi itapata silaha kwa ajili ya operesheni zake za kijeshi nchini Ukraine kutoka Korea Kaskazini, yenyewe ambayo inakabiliwa na vikwazo kwa sababu ya mipango yake ya nyuklia na makombora.

Msemaji wa Kremlin Dmitri Peskov, alisema "Katika kujenga uhusiano wetu na majirani zetu, ikiwa ni pamoja na Korea Kaskazini, jambo muhimu kwetu ni maslahi ya nchi zetu na si maonyo kutoka Washington."

Hata hivyo, ilielezwa kuwa katika ziara hiyo Rais Kim Jong-un aliandamana na maofisa wakuu wa kijeshi, akiwemo waziri wake wa ulinzi na maofisa kutoka vyombo vya uzalishaji silaha na sekta ya teknolojia ya anga.

Kwa mujibu wa wataalamu, mkutano kati ya Vladimir Putin na Kim Jong-un unaweza kuzingatia makubaliano katika uwanja wa silaha, kwa sababu Vladimir Putin anatafuta kupata makombora ya ziada na yanayoangamiza vifaru.

**RFI, BBC**

# NAMUNGO YAIWAHI YANGA DAR

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Yanga ikiondoka leo kwenda Rwanda kwa ajili ya mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Al Merrikh ya Sudan itakayochezwa Jumamosi, kikosi cha Namungo FC kimewasili jijini Dar kuweka kambi ya wiki moja ikiwasubiri mabingwa hao watetezi warejee tayari kwa mchezo wao wa Ligi Kuu Septemba 20.

Ofisa Habari wa Klabu hiyo, Kindamba Namlia amesema awali walitaka kuja Dar es Salaam kwa ajili ya kusaka mechi za kirafiki lakini Bodi ya Ligi ikatoa tarehe ya mechi hiyo ambayo awali haikuwekwa kwenye ratiba.

"Tumepata tarehe mpya ya kucheza dhidi ya Yanga ambayo ni Septemba 20, lakini kwa sababu sisi ni timu ya mpira wa miguu muda wote sisi tuko tayari kucheza, awali tulipanga timu ije Dar es Salaam kwa ajili ya mechi za kirafiki lakini kwa bahati nzuri tumeupata mchezo wa ligi tarehe 20 kwa hiyo hapa ninavyozungumza na wewe timu tayari imeshaingia jijini Dar es Salaam tumeweka kambi, tunafanya mazoezi mara mbili, asubuhi 'gym' na jioni mazoezi ya uwanjani, kama tunaweza kupata mechi yoyote ya kirafiki hapa katikati sawa tutacheza kabla ya mechi yetu dhidi ya Yanga," alisema Kindamba.

Aidha, alibainisha kuwa kikosi hicho ambacho kinafundishwa na Kocha Cedrick Kaze kiko vyema na wachezaji wake wote afya zao ziko vizuri na wanaisubiri kwa hamu Yanga irejee kutoka Rwanda ili wamalizane.

Mpaka sasa Namungo haijashinda mechi yoyote ya Ligi Kuu, ikianza kwa kuchapwa bao 1-0 dhidi ya JKT Tanzania na mechi ya pili ililazimishwa sare ya bao 1-1 na KMC.




Meneja Masoko wa EATV, Edwin Lotti (kulia), akikabidhi zawadi kwa Kikundi cha Barack Obama, ambacho kiliibuka washindi wa mbio namba sita za mbuzi katika mashindano yaliyoandaliwa na Rotary Club Oysterbay, Dar es Salaam ambayo lengo lake lilikuwa ni kutafuta Sh. milioni 320 kwa ajili ya kusaidia elimu, afya na huduma za jamii. **PICHA: EATV**

# COSOTA, TBF zapewa maagizo

**Na Saada Akida**

WAZIRI wa Utamaduni Sanaa na Michezo, Dk Damas Ndumbaro amezitaka bodi za Haki Miliki Tanzania (COSOTA) na Filamu Tanzania (TFB) kuweka mazingira mazuri kwenye tasnia ya sanaa ili kuwa sehemu ya ajira kwa kwa vijana na kuongezea kipato Serikali.

Ndumbaro aliyasema hayo juzi kwenye hafla ya uzinduzi Bodi ya TFB pamoja na mafunzo kwa viongozi hao, iliyofanyika kwenye Hotel ya Onomo, Dar es Salaam.

Ndumbaro, alisema matuamini yake ni kuona muunganiko wa bodi hizo mbili zinasaidia vijana ambao wanatangaza Sanaa na Utamaduni wa Tanzania kuwa ajira kama ilivyokuwa kwenye sekta ya michezo.

Alitolea mfano Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF) na michezo mingine kutoka katoka ridhaa na kuwa ajira ambayo vijana wananufaika na kile wanachokifanya.

"Natarajia muunganiko wa hizi Bodi mbili zitasaidia kukuza uchumi wa nchini kutoka asilimia 19, siku zote watanzania tunachukulia sanaa, Utamaduni na Michezo ni mambo mepesi sana, ila sio hivyo, mnakazi kubwa ya kufanya taasisi mnazosimamia kuongeza ajira na kukuza uchumi wa nchi," alisema Ndumbaro.

Sekta ya Sanaa na utamaduni, mnatakiwa kuumiza kichwa kuhakikisha wanatoka hapo tulipo na kupanda juu pia tukitumia sekta hii kufanya ajira ambayo itawanufaisha wasanii kama ilivyo kwenye mpira wa Miguu," alisema Ndumbaro.

Aliongeza kuwa anaimani viongozi wa Bodi wanauwezo wa kufanikiwa yale anayotaka kuona katika kuongeza uchumi na vijana kunufaika na kazi zao kwa sababu watanzania wanapenda starehe na kula bata.

"Nina imani muunganiko huu Wizara tutapokea simu nyingi kutoka nje kama ilivyo kwa mpira wa miguu, tunapokea simu kutoka mataifa mbalimbali kuelezwa juu ya kuwepo kwa wachezaji watanzania kucheza nje na kutakiwa kujumuishwa katika kikosi cha Taifa Stars.

Pia naomba kuwasisitizia Viongozi kuwa cheo ni dhamana, mnatakiwa kutumia vizuri mamlaka mliyokuwa nayo, kulikuwa na migogoro mingi katika sekta hii ikiwemo suala la maslahi binafsi, sitaki kuona hii migogoro ikiendelea tena," alisema Waziri huyo.

Katika hatua nyingine Waziri huyo aliwataka Mabalozi wa COSOTA akiwemo Msanii Elias Barnaba 'Barnaba' kutumia fursa hiyo kufanya kazi kwa weredi mkubwa ili kutangaza kazi ya Bodi hiyo ndani ya nje ya Tanzania ili wasanii kutambua umuhimu wake.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa bodi ya COSOTA, Victor Tesha alimuahudi Waziri kufanya kazi kwa ushirikiano mkubwa kwa kuangalia usalama wa kazi za wasanii na kukaa na wasanii kuangalia namna bora ya kupata haki zao katika kazi zitakazotumika bila ya ridhaa yao.

"Tumeona hivi karibuni mwanariadha mtanzania Felix Simbu alipata fedha nyingi baada ya kulipwa fidia kutoka moja ya kampuni ambayo ilitumia picha yake, pia hata mshambuliaji wa Simba, John Bocco naye amepata Mamilioni ya fedha baada ya kampuni ya 'Betting' kutumia picha yake pia bila makubaliano," alisema Tesha.

Alisema kama bodi wanahitaji kuona wasanii wananufaika na kazi zao kama alivyoelekezwa na Waziri kwa kuhakikisha wanapata haki zao katika makampuni mbalimbali ambayo yanatumia kazi za wasanii bila utaratibu wa makubaliano.

## Kundemba FC yajivunia kikosi

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

WAKATI leo ikishuka uwanjani kucheza mchezo wake wa kwanza wa ligi kuu ya Zanzibar dhidi ya Jamhuri ya Pemba, benchi la ufundi la klabu ya Kundemba FC limesema linajivunia ubora na uimara wa kikosi chao.

Akizungumza na Nipashe, Kocha wa timu hiyo, Ali Vuai alisema msimu huu wana kikosi cha kazi ambacho wanaamini kitawapa matokeo mazuri kwenye michezo yao ya ligi kuu na wataanza kuonyesha ubora wao kwenye mchezo wa leo.

Alisema kikosi chao hicho wamekifanyia mabadiliko makubwa katika safu ya ushambuliaji na ulinzi kwa kusajili wachezaji wenye viwango vya juu ambao wataipa timu hiyo matokeo mazuri.

Alisema malengo yao makubwa ya kuboresha kikosi hicho ni kuhakikisha wanamaliza ligi wakiwa kwenye nafasi za juu katika msimamo wa Ligi hiyo.

"Tunaenda kuanza mchezo wetu wa kwanza kesho (leo) kwa hamasa kubwa kwa wachezaji na hata mashabiki wetu kwa ujumla, kama tunavyojua michezo ya mwanzo inakuwa na presha kubwa sana ili kuhakikisha kila mtu anapata alama, hivyo na sisi tumejiandaa kutuliza presha yoyote tutakayokutana nayo,"alisema Vuai.

## Baiskeli 'TwendeButiama' wapata mdhamini

**Na Mwandishi Wetu**

WAENDESHA baiskeli mashuhuri wanashiriki ziara maalum ya TwendeButiama kutoka Dar es Salaam kwenda Butiama mkoani Mara kuadhimisha kumbukumbu ya kumuenzi Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere wamepata udhamini kutoka kampuni ya Vodacom.

Tukio hilo la uendeshaji wa baiskeli litakalodumu kwa siku 14, linatarajiwa kufanyika kuanzia Oktoba 1-14 siku ya kumbukumbu ya kifo cha Baba wa Taifa.

Akizungumza na Nipashe mmoja wa waanzilishi wa ziara hiyo ya TwendeButiama' Gabriel Landa, alisema ziara ya mwaka huu inatarajiwa kuwa yenye mafanikio zaidi kutokana na udhamini wa kampuni hiyo ya Vodacom na mpaka sasa tayari waendesha baiskeli 72 wamethibitisha ushiriki wao.

"Safari yetu ambayo ilianza mwaka 2018, inafanya zaidi ya kuadhimisha kumbukumbu ya Baba wa Taifa, tunahamasisha uendeshaji wa baiskeli kitu ambacho Mwalimu Nyerere alikipendelea zaidi katika kuimarisha afya, lakini ziara hii ni kujipambanua kuwa vinara wa kusimamia masuala ambayo mwalimu aliyapambania kama vile elimu, utunzaji wa mazingira na afya bora," alisema Landa na kuongeza,

"Kwa ushiriki wa sekta binafsi na ushirikiano wa waendesha baiskeli, wanaharakati wa mazingira na wataalamu wa afya, mchango wetu unalenga kuenzi maadili ya Mwalimu Nyerere," alisema Landa.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### BARCA YAMTAKA HAALAND
BARCELONA wanapanga kuingia kwenye mbio za kuwania kumsajili mshambuliaji wa Manchester City, Erling Haaland mwakani wakati mchezaji huyo wa kimataifa wa Norway mwenye umri wa miaka 23 anaweza kupatikana kwa pauni milioni 150. **(90min)**

### SILVA AJIPANGA KUSEPA
KIUNGO wa kati wa Manchester City, Bernardo Silva (29), alijadili kuhusu kipengele cha kuachiliwa kwa pauni milioni 50 katika kuongezwa kwa mkataba wake hivi karibuni, huku mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno akifikiria uwezekano wa kuhamia Barcelona msimu ujao. **(Mundo Deportivo)**

### NAGLSMANN AITEGA UJERUMANI
KOCHA wa zamani wa Bayern Munich, Julian Nagelsmann bado yuko chini ya mkataba na klabu hiyo ya Ligi Kuu Ujerumani (Bundesliga), lakini hataomba ada ikiwa Shirikisho la Soka la Ujerumani litataka kumteua kuwa kocha wa timu yao ya taifa. **(Sky Sports)**

### MOYES: SIJAMKATAA LINGARD
BOSI wa West Ham, David Moyes hajamkataa kiungo mshambuliaji wa England, Jesse Lingard mwenye umri wa miaka 30, ambaye ni mchezaji huru na anafanya mazoezi na Wagonga Nyundo hao ili kupata mkataba mpya na klabu hiyo na akiboresha kiwango chake cha mchezo. **(Sports)**

### CHALOBAH BADO YUPO
CHELSEA ilishindwa kumuuza mlinzi wa England, Trevoh Chalobah msimu wa joto na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 hatarajii kuwa na jukumu kubwa katika klabu hiyo atakaporejea kutoka kwa jeraha la nyama za paja hivi karibuni. **(Standard)**

### POGBA MATATANI JUVE
KLABU ya Juventus itaweza kusitisha mkataba wa kiungo wa kati wa Ufaransa, Paul Pogba iwapo nyota huyo wa zamani wa Manchester United atafungiwa baada ya kukutwa na hatia ya kutumia dawa za kusisimua misuli. **(Gazzetta dello)**

### PSG KUIBOMOA MADRID
PARIS St-Germain imetoa orodha fupi ya wachezaji watano wa Real Madrid ambao watawalenga kama kulipiza kisasi kwa klabu hiyo ya Hispania ambayo inamsaka mshambuliaji wa Ufaransa, Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 24. **(Sport)**

### ODEGARARD AFURAHIA ARSENAL
KIUNGO wa kati wa Norway, Martin Odegaard mwenye umri wa miaka 24, alisema "hakuwa na mengi ya kusema" linapokuja suala la mazungumzo ya kurefusha mkataba katika klabu ya Arsenal lakini "nina furaha sana" katika timu hii. **(Nettavisen, via Standard)**

### SARR KUTUA UTURUKI
KLABU za Uturuki zinatayarisha ofa za mkopo kwa mlinzi wa Chelsea Mfaransa Malang Sarr mwenye umri wa miaka 24, kabla ya dirisha lao la uhamisho kufungwa Septemba 15. **(Football Insider)**

### LAMPARD ANUKIA LYON
LYON inafikiria kumteua kocha wa zamani wa Chelsea na Everton, Frank Lampard mwenye umri wa miaka 45, kama kocha wao mkuu baada ya klabu hiyo ya Ligue 1 kumfukuza Laurent Blanc. **(90min)**

### GOMES AKARIBIA FENERBAHCE
KLABU ya Fenerbahce imemwongeza kiungo wa kati wa Everton, Mreno Andre Gomes mwenye umri wa miaka 30, kwenye orodha ya wachezaji wanaowalenga kabla ya dirisha kufungwa. **(Sozcu)**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# SOUTHGATE ASHANGAA WANAOMTUSI MAGUIRE

**Kocha huyo wa England asema kitendo cha mashabiki kumdhihaki...**

**LONDON, England**

KOCHA Mkuu wa Timu ya Taifa ya England, Gareth Southgate ameutaja ukosoaji wa Harry Maguire kama "mzaha" na kudai "matendo ya kipuuzi"anayofanyiwa mlinzi huyo wa Manchester United "ni zaidi ya chochote ambacho nimewahi kuona."

Maguire aliingia kipindi cha pili cha ushindi wa mabao 3-1 katika mechi ya kirafiki dhidi ya Scotland iliyochezwa kwenye Uwanja wa Hampden Park juzi na alidhihakiwa na mashabiki wa nyumbani.

England ilikuwa inaongoza 2-0 kupitia kwa Phil Foden na Jude Bellingham kabla ya Maguire kujifunga bao dakika ya 67 na kuamsha shangwe za kejeli juu yake.

Harry Kane alimaliza pambano hilo kwa bao lake la 59 la kimataifa dakika tisa kabla ya mechi kumalizika huku mashabiki wa England wakiendelea kuimba jina la Maguire kwa kejeli.

Maguire pia alishangiliwa na mashabiki wa Arsenal alipoingia akiitokea benchi kwenye dhidi ya Manchester United iliyochezwa kwenye Uwanja wa Emirates mapema mwezi huu na Southgate anaamini hali hiyo hasi ni zao la kutocheza vizuri.

"Kwa mtazamo wa shabiki wa Scotland, naipata na sina malalamiko kabisa na walichokifanya," alisema Southgate.

"Ni matokeo ya kumdhihaki kwa muda mrefu, kusema ukweli. Lakini ni mzaha. Sijawahi kujua mchezaji anachukuliwa kama yeye, sio na mashabiki wa Scotland lakini na wachambuzi wetu wenyewe.

"Wameunda kitu zaidi ya kitu chochote ambacho nimewahi kuona. Amekuwa mchezaji nguli kabisa katika timu ya pili ya England yenye mafanikio kwa miongo kadhaa.

"Amekuwa sehemu muhimu ya hilo. Nimezungumzia umuhimu wa wachezaji wetu wakubwa, amekuwa muhimu sana. Kila anapokwenda uwanjani, anaonyesha uimara, ni mchezaji bora."

Aliongeza kwa beIN Sports: "Mwitikio usiku wa leo (juzi) ni matokeo ya wajinga kutoka upande wetu ambao wameunda mazingira hayo."

Alipoulizwa jinsi Maguire alivyokuwa, Southgate aliendelea: "Yeye ni mzuri, ni mzuri. Tumekuwa na ushindi mzuri. Amekuwa sehemu kubwa ya hilo. Ameenda na kuzungumza na vyombo vya habari kwa sababu ni aina ya kijana. Yeye yuko mbele. kama anavyofanya siku zote. Sifa kubwa kwa tabia yake."


SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,152,9

MECHI KALI
AL NASR DUBAI
VERSUS
AJMAN CLUB
1 | 2.41
X | 3.47
2 | 2.53

tigo pesa SportPesa
WASHINDI WA MAOKOTO Deilee!
1. Isaya Kajange - 0652 615 XXX
2. Olipa Ngomba - 0652 860 XXX
3. Saidi Isimaili - 0656 268 XXX
4. Yuda Muhami - 0656 331 XXX
5. Shafii Suwedi - 0658 603 XXX
6. Paschal Paschal - 0672 355 XXX
7. Alfani Omary - 0673 986 XXX
8. Godfrey Sanga - 0710 003 XXX
9. Ibrahim Mahende - 0718 790 XXX
10. Johakimu John - 0719 417 XXX
20,000/= KWA KILA MMOJA

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# BARCA YAINGIA VITA KUMWANIA HAALAND



**BARCELONA, Hispania**

MIAMBA ya Hispania, Barcelona inajiandaa katika vita kupigania kumsajili nyota wa Manchester City, Erling Haaland.

Kwa muda mrefu Real Madrid imekuwa ikichukuliwa kama timu inayomfaa zaidi Haaland, lakini sasa kwa mujibu wa tovuti ya michezo 90min, Barca inajiandaa kufanya harakati kumsajili mshambuliaji huyo mahiri, raia wa Norway.

Kwa sasa Barca ina Robert Lewandowski anayeongoza safu ya ushambuliaji, lakini katika mpango wa muda mrefu, Haaland anaonekana chaguo linalofaa kuwa mbadala wa mkongwe huyo wa Poland, ambaye hivi karibuni alitimiza miaka 35.

Mapema mwezi huu ripoti zilisema City inapanga kumpatia Haaland ofa ya mshahara wa pauni 600,000 kwa wiki ikihofia huenda akarubuniwa ahamie klabu za Saudi Arabia au Read Madrid.

Haaland ameng'ara City tangu aliposwasili msimu uliopita akitokea Borussia Dortmund kwa mkataba wa miaka mitano akisaidia timu hiyo kutwaa mataji matatu ambayo ni Ligi ya Mabingwa Ulaya, Ligi Kuu England na Kombe la FA.

Pia yeye Haaland alishinda kiatu cha dhahabu cha Ligi Kuu England na cha Ulaya na pia alitwaa tuzo ya Mchezaji Bora wa Ulaya akimpiku, Lionel Messi.

Kwa jumla Haaland mwenye umri wa miaka 23 amefunga mabao 52 katika mashindano yote msimu uliopita yakiwamo 36 aliyoweka rekodi kwenye Ligi Kuu England.

# Sancho kuondoka United

**MANCHESTER, England**

WINGA wa Manchester United, Jadon Sancho anatarajiwa kuondoka katika klabu hiyo wakati wa dirisha dogo la uhamisho ifikapo Januari, 2024 baada ya kushindwa kumaliza tofauti yake na Kocha, Erik ten Hag.

Sancho amefanya mazungumzo na Ten Hag kuhusu hatima yake United kufuatia kurushiana vijembe kati yao.

Ten Hag alimwondoa winga huyo wa England kwenye kikosi kilichopokea kipigo hivi karibuni kutoka kwa Arsenal na akieleza mtazamo mbaya na uvivu kwenye mazoezi wa Sancho kuwa ndio sababu za maamuzi hayo.

Sancho alijibu kupitia mitandao ya kijamii akikanusha madai hayo na kumshutumu Ten Hag kwa kusema uongo.

Ripoti zimesema hata kukosekana kwa sasa kwa winga mwenzake, Antony kutokana na madai ya unyanyasaji wa wanawake ambayo amekanusha, hakutarajiwi kuongeza nafasi ya Sancho kurejea kwenye kikosi cha kwanza.

Manchester United ilimsajili Sancho mwenye umri wa miaka 22 mwaka 2021 kutoka Borussia Dortmund kwa ada ya uhamisho ya dola milioni 87.94.



911,993/-

# NEEMA YAZIDI KUMWAGIKA LIGI YA NBC CHAMPIONSHIP

**Na Saada Akida**

SHIRIKISHO la Soka Tanzania (TFF), limeingia mkataba wa miaka mitatu na TV3 kwa ajili ya kudhamini Ligi ya NBC Championship wenye thamani ya Sh. milioni 613, imefahamika.

Ligi hiyo ambayo awali ilijulikana kama Ligi Daraja la Kwanza pia inadhaminiwa na Benki ya Taifa ya Biashara (NBC).

Akizungumza na Nipashe jana, Rais wa TFF, Wallace Karia, alisema mkataba huo utakuwa ni maalumu kwa ajili ya kituo hicho cha televisheni kuonyesha mubashara mechi za Ligi ya NBC Championship na anaamini itawasaidia kila kitu kuonekana hadharani. Karia alisema kwa sasa watafanikiwa kuona timu ambazo zinajihusisha na vitendo viovu kwa ajili ya kujinufaisha lakini watapata nafasi ya kubaini malalamiko ya baadhi ya klabu zinazofanyiwa makosa.

"Ninaimani wadhamini wetu hawatajutia kabisa kufanya kazi pamoja na TFF katika kubeba dhamana ya kuonyesha mubashara mechi zetu za Championship kwa msimu huu.

Kuonekana kwa Ligi Kuu Bara kupitia Azamtv imekuwa hamasa kubwa na kuifanya iwe bora, matarajio yangu kwa mkataba huu tulioingia na TV 3 kwa ajili ya kuonyesha mechi ya Championship itafanya pia kuwa bora zaidi na kuleta wadhamini wengine," alisema Karia.

Aliongeza udhamini huo utaongeza hamasa kwa timu za Ligi ya Championship kujiandaa vyema ili zipande daraja na kwenda kuonekana katika ligi nyingine ya daraja la juu (Ligi Kuu Bara).

"Tutakuwa wakali kwa klabu ambazo hazikujiandaa kucheza daraja la juu, niwaombe wapambane kutafuta wadhamini ili kujimudu katika ligi wanayoshiriki, TFF sio kazi yao kuwatafutia klabu wadhamini, hilo ni jukumu la uongozi wa klabu hizo," Karia alisema.

Naye Msimamizi wa TV3, Emmanuel Sekawa, alisema mkataba huo ni hatua kubwa kwao kwa sababu wanatarajia kuonyesha mechi 170 kati ya 240 ambazo zitachezwa katika ligi hiyo msimu huu.

"Tunatarajia Ligi ya Championship itaonekana katika mataifa mbalimbali ikiwamo Kenya, Uganda, Rwanda , Afrika Kusini, Uganda na Msumbiji, lengo la kutangaza ligi hii na wachezaji kuonyesha vipaji vyao na kuonekana kujiuza kwa kutazamwa," alisema Sekawa.

## Ushindi wa Simba

INATOKA UK. 24

owasaidia 'kumaliza' mchezo huo wa ugenini.

"Tulifanikiwa kucheza na timu hiyo kwa kushinda, ninaimani kufikia mechi ijayo watakuwa kivingine, nawatumia wachezaji wangu hawa wawili kueleza nini wanachokifahamu kwa wapinzani wetu wanapokuwa kwenye uwanja wa nyumbani.

Haitakuwa mechi rahisi, kama tulivyowafunga katika tamasha letu haitaleta maana wao ni wepesi, ninaimani watakuja tofauti na vile walivyocheza awali kwa sababu haya mashindano," alisema Robertinho.

Aliongeza mchezo huo ni wa mashindano na wanataka kufanya vizuri katika mechi hizo mbili na kusonga mbele akiamini Chama na Phiri, watatoa siri za timu hiyo inapocheza nyumbani.

Kocha huyo alisema maandalizi ya timu yake yanaendelea vizuri na tayari ameyafanyia kazi mapungufu ya kila eneo na kuboresha pale walipofanya vizuri kwa kuzingatia michezo mitatu ya kirafiki waliocheza hivi karibuni.

Naye Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema maandalizi muhimu kuelekea mechi hiyo ya kimataifa yamekamilika na hakuna kitakachowazuia kutinga hatua ya makundi, kusaka robo na kufikia malengo yao ya kucheza nusu fainali.

"Tumecheza michezo mitatu ya kirafiki wakati wa maandalizi, Kocha Robertinho ameridhishwa na muunganiko wa kikosi, tupo imara, kiufundi tupo vizuri," Ahmed alisema.

Aliongeza wachezaji wote wako katika hali nzuri na nyota waliokuwa kwenye timu za taifa wamesharejea na wameungana na wenzao.

Alisema pia uongozi umefurahishwa na mwitikio mkubwa wa mashabiki waliojitokeza kwenda kuishangilia timu yao katika mechi hiyo ya kimataifa.

## Yanga yaifuata Al Merrikh

INATOKA UK. 24

kwenye hii michuano, ila msimu huu inatakiwa wajipange vizuri kama sisi tulivyojipanga, dakika 90 za pale Kigali ndizo zitatupa nini kitakuja kutokea katika mechi ya marudiano jijini Dar es Salaam, tunajua utakuwa mchezo mgumu sana lakini tuna imani kubwa na benchi letu la ufundi, tuna imani kubwa na wachezaji wetu.

Pia tuna imani kubwa ya hamasa ya wanachama na mashabiki wetu ambao watasafiri kutoka Dar kwenda nchini Rwanda kwa ajili ya mechi hiyo kwa sasa hesabu ya haraka haraka ni jumla ya wachezaji 36 wamejaa, lakini kuna mashabiki ambao wapo maeneo ya mipakani ambao wanasema watasafiri asubuhi siku ya mechi na kurejea baada ya kumalizika," alisema Kamwe.

Aliongeza amewataka wanachama na mashabiki kutokuwa na hofu na tayari wameshafanya mawasiliano kwa ajili ya wote watakaokuwa Kigali kupata nafasi ya kuingia uwanjani kushuhudia mchezo huo wa kimataifa.

"Tumezungumza na Shirikisho la Soka Rwanda, pamoja na klabu ya Al Merrikh, wameshatutumia bei za tiketi na majukwaa yake, utaratibu utakuwa mzuri kila shabiki wetu kuiona timu," Kamwe alisema.

Naye kiungo wa timu hiyo, Maxi Nzengeli, aliyechaguliwa kuwa mchezaji bora wa Ligi Kuu mwezi uliopita amewashukuru Wanayanga wote pamoja na mashabiki wa soka nchini ambao wamekuwa mchango kwa yeye kupata tuzo hiyo.

Nzengeli amesema tuzo hiyo imekuwa kama chachu ya yeye kulazimika kufanya mambo makubwa zaidi ili kuendelea kuwafurahisha mashabiki wake, pamoja na kuipatia ushindi timu yake.

"Nashukuru Mungu kwa kupata tuzo hii, nalishukuru benchi la ufundi, na wachezaji wenzangu wote, viongozi wote pamoja na mashabiki wote, inanipa moyo wa kuendelea kujituma na kufanya vizuri ili nipate tena tuzo siku zijazo," Nzengeli alisema.

Tayari serikali kupitia Naibu Waziri wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Hamisi Mwinjuma 'Mwana FA' imesema inahitaji kuona timu hizo zinakwenda kupambana na kupeperusha vyema bendera ya Tanzania.

Mwana FA amesema anataka kuona ushirikiano unaongezeka wakati timu hizo zinashiriki katika michuano hiyo ya kimataifa na anaamini wamefanya maandalizi mazuri.

Waziri huyo alisisitiza anataka kuona mabadiliko kwa klabu hizo mbili kuweka pembeni tofauti zao wanaposhiriki mashindano hayo ya kimataifa kwa sababu wanataka kuona timu zote mbili zinasonga mbele.


SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01.16/09/23 | 17:00 | Bristol City vs West Bromwich Albion | 2.41 | 3.25 | 2.80 |
| 02.16/09/23 | 17:00 | Kilmarnock FC vs Hibernian FC | 2.48 | 3.30 | 2.70 |
| 03. 16/09/23 | 17:30 | Rio Ave FC vs FC Famalicao | 2.50 | 3.15 | 2.70 |
| 04. 16/09/23 | 19:00 | Inter Milano vs AC Milan | 2.16 | 3.35 | 3.15 |
| 05. 16/09/23 | 19:30 | VfL Bochum vs Eintracht Frankfurt | 2.80 | 3.50 | 2.27 |
| 06. 16/09/23 | 20:00 | USL Dunkerque vs Grenoble Foot | 2.65 | 3.10 | 2.60 |
| 07. 16/09/23 | 20:00 | Rodez Aveyron Football vs Angers SCO | 2.70 | 3.15 | 2.55 |
| 08. 16/09/23 | 20:00 | Paris FC vs Amiens SC | 2.55 | 3.15 | 2.70 |
| 09. 16/09/23 | 20:30 | SK Sturm Graz vs FC Salzburg | 2.70 | 3.30 | 2.24 |
| 10. 16/09/23 | 21:45 | Cardiff City vs Swansea City | 2.55 | 3.25 | 2.65 |
| 11. 17/09/23 | 13:30 | Cagliari Calcio vs Udinese Calcio | 2.85 | 3.25 | 2.39 |
| 12. 17/09/23 | 15:00 | Getafe CF vs CA Osasuna | 2.50 | 2.90 | 2.95 |
| 13. 17/09/23 | 15:30 | FC Twente Enschede vs Ajax Amsterdam | 2.65 | 3.35 | 2.48 |
| 14. 17/09/23 | 16:00 | Frosinone Calcio vs Sassuolo Calcio | 2.75 | 3.35 | 2.40 |
| 15. 17/09/23 | 16:30 | FC Heidenheim vs Werder Bremen | 2.27 | 3.70 | 2.70 |
| 16. 17/09/23 | 17:15 | US Catanzaro vs Parma Calcio | 2.42 | 3.00 | 2.65 |
| 17. 17/09/23 | 19:00 | ACF Fiorentina vs Atalanta BC | 2.35 | 3.45 | 2.75 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

ALHAMISI - 14/09/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 00:00 | 2814 | Ararat Yerevan vs Shirak Gyumri | 1.82 | 3.26 | 4.08 |
| 16:00 | 5818 | KF Tirana vs Skenderbeu | 1.83 | 3.35 | 3.91 |
| 16:30 | 3913 | Al Ain vs AL Bataeh (UAE) | 1.53 | 4.48 | 4.48 |
| 16:30 | 4578 | Emirates Club vs AL Wahda Scc (UAE) | 4.69 | 4.38 | 1.52 |
| 17:00 | 5936 | CA Union Santa Fe Reserve vs CA Platense | 2.32 | 3.09 | 2.89 |
| 18:00 | 1372 | MC El Bayadh vs CS Constantine | 4.37 | 3.86 | 1.63 |
| 18:00 | 2545 | US Khenchela vs ES Setif | 2.70 | 3.51 | 2.25 |
| 18:00 | 2715 | Nc Magra U21 vs Js Kabylie | 3.36 | 3.31 | 2.00 |
| 18:00 | 2961 | AL Akhdood vs Al Ittihad Jeddah | 11.49 | 6.06 | 1.22 |
| 18:00 | 3509 | US Oued Souf vs Cr Belouizdad | 5.69 | 4.16 | 1.46 |
| 18:00 | 3549 | Js Saoura vs US Biskra U21 | 1.61 | 3.68 | 4.80 |
| 18:00 | 4072 | AC Paradou vs Usm Alger | 2.96 | 3.21 | 2.22 |
| 18:00 | 4776 | MC Alger vs ES Ben Aknoun | 1.32 | 4.38 | 8.97 |
| 18:20 | 1877 | Hajer Club vs Jeddah Club | 2.38 | 2.98 | 2.82 |
| 18:20 | 4743 | AL Safa (Sa) vs AL Arabi (SA) | 8.20 | 4.90 | 1.26 |
| 18:30 | 1226 | Vidar vs Madla | 1.24 | 6.07 | 7.08 |
| 18:45 | 2168 | AL Bukayriyah FC vs Ohud Medina | 2.17 | 3.09 | 3.09 |
| 19:00 | 4904 | UD Rayo Ibense vs CD Castellon B | 2.73 | 2.93 | 2.49 |
| 19:00 | 5051 | Vllaznia vs Partizani Tirana | 4.06 | 3.55 | 1.75 |
| 19:00 | 5760 | Al Nasr Dubai vs Ajman Club | 2.41 | 3.47 | 2.53 |
| 19:05 | 5926 | Al Orubah vs AL Baten | 1.98 | 3.23 | 3.38 |
| 19:15 | 5624 | Hapoel Petach-Tikva W vs Hapoel Raanana W | 1.88 | 3.97 | 3.15 |
| 19:30 | 1556 | Hapoel Acre vs Maccabi Herzliya | 1.98 | 3.48 | 3.48 |
| 19:30 | 1750 | Bnei Yehuda vs Ironi Tiberias | 2.75 | 3.27 | 2.44 |
| 19:30 | 1826 | Hapoel Rishon Lezion vs Ironi Kiryat Shmona | 3.52 | 3.57 | 1.94 |
| 19:30 | 5001 | Hapoel Ramat Gan vs Sectzya Nes Ziona | 4.00 | 3.79 | 1.77 |
| 19:30 | 5105 | Ironi Hasharon vs El Fahem | 2.75 | 3.11 | 2.54 |
| 20:00 | 2842 | Aso Chlef vs MC Oran | 1.38 | 4.48 | 6.51 |
| 20:00 | 4767 | Maccabi Kishronot Hadera W vs Bnot Netanya W | 1.49 | 4.48 | 4.89 |
| 20:00 | 5128 | HB Koge vs Kolding IF | 3.53 | 3.53 | 1.84 |
| 20:30 | 1911 | AS Tel Aviv University W vs Hapoel Nir Ramat Hasharon W | 1.17 | 6.50 | 11.17 |
| 20:30 | 3839 | Al Faisaly (KSA) vs Al Jabalain | 1.88 | 3.23 | 3.73 |
| 20:45 | 4890 | Kfum 2 vs Follo | 9.92 | 6.68 | 1.16 |
| 20:45 | 5787 | Duque de Caxias RJ vs Portuguesa RJ | 3.82 | 3.36 | 1.85 |
| 21:00 | 5868 | Al Wehda vs Dhamk | 2.10 | 3.45 | 3.29 |
| 21:15 | 5295 | Westerlo U21 vs AS Eupen U21 | 3.57 | 3.98 | 1.76 |
| 23:00 | 2619 | Comerciantes Unidos vs CS Union Huaral | 1.22 | 5.25 | 9.90 |
| 23:00 | 3122 | Vargas Torres vs 9 De Octubre FC | 2.40 | 2.86 | 3.01 |

IJUMAA - 15/09/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 00:00 | 1956 | Orsomarso vs Real Santander | 2.65 | 2.90 | 2.50 |
| 00:00 | 3025 | Indigenas de Matagalpa FC vs Managua FC | 3.72 | 3.46 | 1.84 |
| 00:30 | 1724 | Deportes Tolima vs Independiente Medellin | 2.17 | 3.11 | 3.16 |
| 00:30 | 2607 | Londrina PR vs Ituano SP | 2.37 | 2.90 | 3.00 |
| 01:00 | 1537 | CA Platense vs Lanus | 2.54 | 2.81 | 2.86 |
| 01:00 | 2730 | Santos vs Cruzeiro | 2.42 | 2.99 | 2.84 |
| 01:00 | 3483 | Fortaleza CE vs Corinthians | 1.66 | 3.48 | 4.80 |
| 01:00 | 3983 | Colo Colo vs Copiapo | 1.38 | 4.48 | 6.51 |
| 01:00 | 5406 | Huachipato vs CD Palestino | 2.43 | 3.21 | 2.65 |
| 01:45 | 5685 | Rionegro Aguilas vs Union Magdalena SM | 1.50 | 3.72 | 6.11 |
| 02:00 | 5974 | Coritiba vs Bahia BA | 2.27 | 3.18 | 2.89 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Alhamisi Septemba 14, 2023
Nipashe



Southgate ashangaa wanaomtusi Maguire UKURASA 21

# YANGA SC YAIFUATA AL MERRIKH KIBABE

## ●●●Nzengeli aahidi makubwa, uongozi wawatoa hofu mashabiki...

**Na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha Yanga kinatarajia kuondoka nchini leo kuelekea Rwanda kwa ajili ya kuwafuata Al Merrikh kutoka Sudan katika mechi ya kwanza ya hatua ya kwanza ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika itakayochezwa Jumamosi kwenye Uwanja wa Pele Kigali, imeelezwa.

Mechi ya marudiano ya timu hizo itachezwa Septemba 29, mwaka huu kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam na mshindi wa jumla atatinga hatua ya makundi ya michuano hiyo inayosimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, alisema anaamini mechi hiyo itakuwa ngumu kwa sababu timu wanayocheza nayo ni kubwa na ina uzoefu katika michuano hiyo.

Kamwe alisema pia kila upande umejiandaa vyema kusaka matokeo chanya katika mechi ya kwanza na kujiweka kwenye mazingira bora kuelekea mchezo wa marudiano.

Alisema wachezaji wao wamejipanga kucheza katika kiwango bora katika dakika 90 za mechi ya kwanza kwa sababu wanataka kufikia malengo.

"Hatuna tatizo na Al Merrikh, tunatambua ni klabu kubwa, kongwe na huwa inafanya vizuri

INAENDELEA UK. 23



Winga wa Yanga, Maxi Nzengeli (mbele), akipambana kuwania mpira dhidi ya Attohoula Yao katika mazoezi ya timu hiyo yaliyofanyika kwenye Uwanja wa Avic ulioko Kigamboni, Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

# USHINDI WA SIMBA UTAPATIKANA HAPA

**Saada Akida**


UNGO Clatous Chama na Moses Phiri, ambao ni raia wa Zambia wamekabidhiwa 'mikoba maalumu' ya kuhakikisha Simba inapata matokeo chanya katika mechi yake ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya wenyeji, Power Dynamos itakayofanyika keshokutwa kwenye Uwanja wa Levy Mwanawasa uliopo Ndola nchini humo.



Kikosi cha Simba kinatarajia kuondoka nchini leo tayari kuwavaa Wazambia hao katika mechi ya kwanza ya hatua ya kwanza itakayochezwa kuanzia saa 10:00 jioni.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Mkuu wa Simba, Roberto Oliviera "Robertinho", alisema licha ya kucheza na Power Dynamos na kupata matokeo mazuri katika mechi ya kirafiki, lakini bado anahitaji kuwajua zaidi wapinzani wao ambao watakuwa nyumbani.

Robertinho alisema kazi kubwa ambayo amewapa Chama na Phiri ni kutoa siri ya Power Dynamos wanavyocheza mechi za nyumbani ili waingie na mbinu itakay-



INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >